# *Kuchunga Kanisa la Mungu*

JEFF VANGOETHEM

AUTHENTICITY BOOK HOUSE
in partnership with twelve21 GLOBAL

Mfululizo wa Uchungaji: Kitabu cha Kwanza

*Kuchunga Kanisa La Mungu*
Hakimiliki© 2019 kwa Jeff VanGoethem
Mhariri mchangiaji: Dianne L. Taylor

ISBN (4 x 6 paperback): 13: 978-1-943004-38-6
ISBN (eBook): 13: 978-1-943004-40-9

Authenticity Book House
Winterset, IA 50273
www.ABHBooks.com
abhinfo@abhbooks.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutumia sehemu ya kitabu hiki au kutoa nakala kwa namna yoyote, taswira, kieletroniki, au kwa njia zinginezo, ambazo ni pamoja na kutoa nakala, kurekodi, unasaji aukutumia mfumo wowote wa utunzaji taarifa bila idhini ya kimaandishi ya mtoaji wa kitabu isipokuwa tu katika nukuu fupi zitumiwazo katika makala na upembuzi yakinifu.

*Wahusika wote kwenye chapisho hili, isipokuwa wale wanaotokana na Maandiko au kwenye orodha ya marejeleo, ni wa kubuni na kama kuna hali ya kufanana kwa namna yoyote ile na watu halisi, walio hai au wafu, ni bahati tu iliyojitokeza tu.*

Nukuu zote za maandiko, isipokuwa vinginevyo kwa kuelekeza, zimenukuliwa kutoka kwenye Biblia ya Swahili Union Version, hakimiliki © 1952, 1997: Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

Kwa sababu ya hali ya kubadilika badilika kwa mtandao wa internet, anwani yoyote ya tovuti au dokezo kwenye kitabu hiki vyaweza kuwa vimebadilika tangu kitabu kitolewa au haifanyi kazi tena.

Mbunifu wa jalada: Schechner & Associates
Mpangilio: Schechner & Associates

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1
Kimetolewa na Authenticity Book House, kwa ubia na Twelve21 Global
*Kimechapishwa nchini Marekani*

## Huduma ya Authenticity Book House

Authenticity Book House (ABH) hutoa **vijitabu vidogo kwa ajili ya mafunzo ya wachungaji**. Tunasambaza vitabu vyenye fundisho linalokubalika kitheolojia kwa wachungajia ambao wana mafunzo kidogo au hawana kabisa mafunzo ya kina ya Biblia. ABH hurahisisha Yaliyomo ili kufikia kiwango stahiki cha usomaji bila kupunguza uzito wa kweli muhimu zinazohitajika kwaajili ya mambo ya kiroho na uongozi.

Umbo dogo la vitabu vyetu hurahisisha usafirishaji na utoaji kwa bei nafuu. Kwakuwa vitabu hivi husafiri zaidi ya kile kituo cha kwanza kilicholengwa, tunaambatanisha ujumbe injili unaoeleweka, tukizisambaza habari njema kwa kadiri ya umbali ambao kitabu kitaenda.

Mfumo wetu wa utoaji wa vitabu ni wa ushirikiano wa kundi ambalo ni pamoja na wanatheolojia na waliothibitishwa wahariri, waandishi wabobevu na wafasiri, na washauri waelekezi juu ya tamaduni.ABH iv Kuhusu ABH inakusudia kutoa mtaala kamili kwaajili ya kuwajengea wachungaji uwezo. Tunatoa machapisho mengine pia ili kuwezesha huduma

yao kuwafikia maaminio wapya na washirika walio katika hali ya kurudi nyuma.

# ORODHA YA YALIYOMO


Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .1

Sura ya Kwanza: Hitaji la Dharula . . . . . . . . . . . . . . . . .5

Sura ya Pili: Wito wa Kuongoza . . . . . . . . . . . . . . . . . .21

Sura ya Tatu: Utambulisho Mpya . . . . . . . . . . . . . . . . .29
Mzee ni nani? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .31
Mwangalizi ni nani? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .33
Mchungaji ni nani? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .39

Sura ya Nne: Rafiki Mpya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .51

Sura ya Tano: Hali ya Ibada Binafsi ya Mchungaji . .59
Ibada Binafsi kwa Mungu katika Maombi. . . . . . .59
Ibada Binafsi kwa Mungu katika Neno . . . . . . . . .66
Kutoa Mwongozo wa Kiroho kwa Wengine . . . . .70

Sura ya Sita: Tabia ya Mchungaji . . . . . . . . . . . . . . . . .81
Shauku Njema . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .82
Vigezo vya Ujumla . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .84
Mahusiano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .89
Ukomavu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .91

Sura ya Saba: Mfano wa Mchungaji . . . . . . . . . . . . . .103

Hitimisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 117

Dondoo za Mwisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .119

# Utangulizi

Miaka kadhaa iliyopita, niliingia kwenye nchi moya ya kiafrika kwenye moja ya safari zangu za utumishi ndani bara hili. Niwasili kwenye uwanja wa ndege, ambako hugeuka kuwa tukio lenye mrorongo mrefu kwa kuwa maafisa wa uwanja wa ndege hukagua mizigo mara kwa mara ili kuhakikisha hakuna kitu cha hatari na cha kutilia shaka ambacho kinapitishwa na kuingizwa nchini mwao. Nilikuwa na matarajio, kama ilivyo kawaida, kupita kwenye mchakato huu wa ofisi za uhamiaji kwa haraka iwezekanavyo. Nchi hii ilikuwa inapitia machafuko ya kisiasa na kiuchumi kwa wakati huo ambao niliitembelea, na watu wake waliathiriwa kwa kiasi kikubwa sana.

Nilipoanza kusogea mbele, hali nikitarajia kujiunga kwenye mstari mrefu kisha kuingia kwenye zoezi la kusubiri kwa muda mrefu. Nilitazama juu, nikashtushwa kumuona mwanaume mmoja mwenye umbo kubwa amevalia vazi la suti ya rangi ya buluu akiwa amebeba mkononi mwake kibao kidogo kilichoandikwa jina langu. Sikuweza kumtambua kwa mara moja japokuwa nimeitembelea nchi hii na viwanja vyake vya ndege mara kadhaa

hapo awali. Nikajiuliza, Huyu ndugu ana nini nami?

Kumbe huyu ndugu alikuwa ni afisa wa jeshi wa serikali ya nchi hiyo. Alijitambulisha kwangu, akajieleza ya kwamba yeye ni rafiki wa mchungaji ambaye amenialika. Nilijikuta nikihudumiwa kwa haraka kuelekea kwenye taratibu za uhamiaji ndani ya muda mfupi, afisa huyu wa jeshi alinibebea mizigo yangu na kunisaidia kwenye mahitaji yangu. Kila mmoja pale kwenye viwanja vya ndege alinitazama kwa jicho la utofauti, kama vile mgeni mwenye hadhi maalum. Mapokezi ya hadhi hii sijawahi kupewa mara kwa mara!

Baada ya kukamilisha taratibu zote kwenye ofisi za uhamiaji na kusalimiana na mchungaji ambaye ni mwenyeji wangu, nilimgeukia yule afisa wa jeshi ambaye alikuwa akinisaidia kwenye zoezi lote hilo na kumuuliza kwanini nimepewa kiwango kikubwa cha ukarimu kiasi kile. Yule afisa wa jeshi alinijibu ya kwamba mchungaji alimtendea mambo mema. Kwa hiyo alitaka kurudisha shukurani zake.

Baadaye nilikuja kufahamu ya kwamba kanisa analoliongoza yule mchungaji liliufikia mtaa ambao afisa yule wa jeshi alikuwa anaishi na kufanya sherehe kubwa kwa ajili ya watoto

kipindi cha sikukuu ya Krismasi, na kuwapatia watoto zawadi. Afisa huyu wa jeshi aliheshimu sana tendo lile la kanisa. Kwa sababu hiyo alianza kuhudhuria kwenye kanisa la yule mchungaji na kutaka kujua kuhusu maswala ya imani ndani ya Kristo.

Japokuwa alikuwa na cheo kikubwa lakini afisa huyu alikuwa na maumivu kwenye moyo wake kama wanadamu wengine wa kawaida na alipambana na maswali mengi binafsi juu ya changamoto za kimaisha. Ukarimu wa mchungaji na kanisa iliyagusa maisha ya ndugu huyu na kumsogeza karibu.

Ninaamini katika kanisa, ninaamini katika injili, na ninaamini katika upendo wa Mungu. Watu huja kwenye kanisa la Mungu kupitia njia mbalimbali, mlango wa ukarimu ni moja ya milango hiyo ya kuwavuta watu. Lakini baada ya watu hawa kuja kanisani tunawatendea nini? Ni kwa namna gani tunaweza kuwatunza na kuwachunga kama sehemu ya kundi zizini mwa Mungu? *Kazi ya mchungaji ni nini?*

Nimeona makanisa mengi yanayokua ndani ya bara la Afrika. Ni jambo linaloleta furaha, ni sehemu ya ushuhuda wa utendaji wa Mungu huko. Shauku ya kutaka kuleta mchango kiasi kwa wachungaji ambao wanatenda kazi bila

kuchoka na wenye moyo wa kujitoa ambao ninakutana nao kwenye nchi mbalimbali ndiyo hunichochea kurudi Afrika mara kwa mara.

Nimetumika kama mchungaji kwa zaidi ya miaka theathini na mitano na, ikimpendeza Bwana, nitaendelea. Mungu alinibariki kupata mafunzo ya muhimu na muda wote wa maisha ya uchungaji hali nikijifunza. Ninaamini mawazo nitakayowasilisha kwenye kitabu hiki yatakuwa msaada kwa wachungaji wote kuyatafakari maswali haya, "Uchungaji ni nini?" na "Ni kwa namna gani wachungaji huchunga watu?" Habari ifuatayo, ambayo ninaisimulia kupitia mtu wa kufikirika aitwaye Immanuel, iwe baraka na msaada kwa kila aisomaye.

# Sura ya Kwanza:

## Hitaji la Dharula

Kijana Immanuel alikuwa akivuna mihogo kutoka kwenye ardhi iliyokauka, jasho likimtiririka kutokana na ukali wa jua la msimu wa kiangazi. Kikapu kilianza kuwa kizito kwa mavuno kuashiria ya kwamba muda si mrefu anaweza kumpeleka mama yake kisha akaelekea mtoni. Kijiji alichokuwa anaishi Immanuel kilikuwa mbali na miji mikubwa, lakini kulikuwa na shughuli nyingi za kimaisha zikiendelea huko na kumshughulisha kijana huyu – uvuvi, ukulima wa mazao kwenye mashamba ya nyumbani kila msimu, hasa kipindi ambacho kulikuwa na msimu mzuri wa mvua, na alimsaidia mama yake na shughuli za nyumbani. Alifurahia pia kwenda shule pamoja na rafiki zake. Kwa kifupi Immanuel alikuwa anajivunia sana kaya yao pale kijijini.

Immanuel alipokelewa na uso wa furaha kutoka kwa mama yake mzazi alipotua kikapu cha mihogo kwenye sehemu ya kukokea moto kabla hajaelekea kukutana na rafiki zake. Mama yake amemlea na kumfundisha mambo mengi ya kimaisha kama vile maswala ya kujitambua.

Kwa mfano, amewahi kumfundisha juu ya namna alivyopewa jina hilo Immanuel, ya kwamba lilitokana na yeye kuzaliwa siku ya Krismasi. Immanuel alikuwa hajui sana kuhusiana na mambo ya Krismasi zaidi ya kujua ya kwamba kanisa huisherehekea hii kama sikukuu, na pia alitambua kuwa ndiyo chanzo cha jina lake.

Kwenye mawazo ya Immanuel hakukuwa na maswala ya kanisa kama ilivyokuwa maswala ya uvuvi. Lakini mama yake mzazi alihudhuria ibada nyingi za sikukuu kanisani. Alikuwa na marafiki zake huko. Immanuel alijifunza mambo machache ya kanisa kwa kumsikiliza mama yake alipokuwa anasimulia. Kwa mfano, alitambua ya kwamba miaka kadhaa iliyopita kuna watu waitwao wamishonari walikuja kijijini kwao na kujenga kanisa. Alijua habari hii lakini haikuwa na maana yoyote kwake kwakuwa hakuwa anaelewa maana ya umishonari.

Immanuel alivutiwa na uimbaji kila alipokuwa anapita kando ya kanisa, lakini bado, hakuweza kuingia ndani. Mchungaji ambaye alikuwa ni mzee alikuwa akiishi ng'ambo ya pili ya kijiji kile. Immanuel hakuwa anamjua sana mchungaji yule. Ukilinganisha na shughuli zingine zilizokuwa zinaendelea pale kijijini kijana huyu hakuvutiwa na mambo ya kanisa.

Misimu ilivyokuwa ikibadilika, Immanuel aliweka umakini wake kwenye kujiendeleza kimasomo kwenye shule ya kijiji. Baba yake alimlipia karo ya shule kutokana na faida za shughuli zake za ufugaji wa ng'ombe na mbuzi. Immanuel alijifunza kwa uharaka sana kusoma. Walimu wake walikuwa wakimuita mbele ya darasa kusoma kwa sauti.

Swala la shule kwake lilifikia mwisho akiwa na umri wa miaka kumi na tatu alipotolewa shuleni ili amsaidie baba yake kuchunga mifugo. Lakini aliendelea kusoma kila kitu chenye maandishi kilichokuwa mbele yake iwe ni kitabu, gazeti, kipande cha karatasi au kitu chochote. Alikuwa ni kijana mwenye shauku kubwa sana ya maneno na kujifunza.

Baada ya miaka kadhaa, Immanuel alikuwa kijana mkubwa mwenye afya na mwonekano thabiti. Watu kijijini walianza kumtambua kama kijana mwenye umakini na na asiyepoteza muda linapokuja swala la kuchunga mifugo ya baba yake. Maisha yake kwa ujumla kwa sasa yalikuwa yameelekezwa kwa hawa mifugo na muda kidogo wa kujisomea ambavyo vilimletea hali ya ridhiko. Hata hivyo siku moja kuna ombi moja alilipokea kutoka kwa mama yake mzazi nalo liliyabadilisha maisha yake siku zote.

“Immanuel, unaweza kuambatana nami kanisani kwenye sikukuu ya Pasaka? Kutakuwa na ibada maalum sana imeandaliwa na ugeni wa mmishonari mmoja.”

Hali ya udadisi na kutaka kujua zaidi ikaibuka ndani ya Immanuel. “Kwani mmishonari ni nani?”

“Kwa kweli sijui,” mama yake alijibu. “Amesafiri kutoka nchi ya ng’ambo kuja huku kwetu, ninadhani hivyo. Hebu wewe twende wote kanisani.”

Immanuel alikubaliana na ombi la mama yake. Alipendelea kujifunza vitu vipya na kijiji chao hakikuwa na mahusiano na watu wowote kutoka nchi za ng’ambo.

Siku ya Jumapili ya Pasaka, Immanuel na mama yake walijionea umati mkubwa wa watu waliokuwa wakiingia kanisani – kama watu wazima arobaini hivi, na watoto wengine wamejikusanya mbele ya kanisa. Nyimbo zilitamalaki kanisani huku Immanuel akitazama huku na kule. Alitazama mbele ya kanisa, sehemu inayoheshimika sana, alikuwa ameketi mtu mmoja aliyevalia mavazi nadhifu. Immanuel alijitahidi kukodoa macho ili amuone vizuri mtu yule. Lakini kanisa lao la muda mrefu, lisilo na madirisha, lililokuwa na matobo kwenye bati yenye kupenyeza mwanga,

lilimzuia Immanuel kumuona yule mtu aliyeketi mbele kama ambavyo angetamani. Alijaribu kuyachezesha macho yake huku na kule ili aone vizuri, na ndivyo yalivyokuwa mawazo ya watoto waliokuwa wamekaa mistari ya mbele. Macho yao yalielekezwa kwa mgeni aliyewatembelea. Immanuel alimuona yule mgeni akitoa tabasamu na kufurahia uimbaji uliokuwa ukiendelea.

Hatimaye ukafika wasaa wa yule mgeni kusimama na kuongea, aliongea kwa kutumia lugha ngeni. Mwalimu mmojawapo kutoka shule ya kijiji alisimama na kutasfiri.

"Ni wangapi wenu wanajua umuhimu wa sikukuu hii?" yule mgeni aliuliza. "Ni wangapi wenu wanajua nini hasa maana ya Pasaka?"

Immanuel alisikia minong'ono ya kukubaliana na akaona vichwa vikitikiswa kama ishara ya kukubaliana na yale maswali ya mgeni. Hakuwa na utulivu binafsi. Kwanza, mkao wa kanisani ulikuwa ni kitu kigeni kwake. Pili, alikuwa hajui jibu sahihi la kumpatia mgeni juu ya yale maswali aliyouliza. Aliamua kuachana na mawazo yaliyokuwa yanaendelea kichwani mwake ili amskilize muhubiri ambaye alikuwa ameanza kusimulia kisa fulani kama njia ya kujibu maswali yake mwenyewe.

"Pasaka inatukumbusha wakati ambapo Yesu, mwana wa Mungu, alipokuja duniani miaka mingi iliyopita. Baba yake, Mungu, alimtuma na hali akiwa duniani aliishi maisha makamilifu. Hakuishi kama ambavyo sisi tunaishi, kwani sisi tunatenda dhambi kila iitwapo leo. Yesu aliishi bila kutenda dhambi, ni mwanadamu pekee aliyewahi kuishi maisha ya namna hiyo. Hakumkosea wala kuwa kwazo kwa mtu awaye yote."

Immanuel alishituka kidogo kwakuwa alikumba dhambi yake mojawapo – kuna wakati yeye na rafiki yake waliiba pombe kwenye nyumba ya mwanakijiji mmoja na kunywa kisha wakalewa chakali. Hakuna mtu ambaye wamewahi kumsimulia juu ya hilo. Kuna hali ya kukosa amani ikamuingia ndani yake. Alijisikia hatia. Akatambua wazi ya kwamba anaishi maisha tofauti na yale ambayo Yesu aliyaishi. *Yesu hakutenda dhambi wala hakuwa kwazo kwa mtu yeyote.* Immanuel alijitambua ya kwamba yeye ametenda yote mawili. Alitambua wazi ya kwamba japokuwa watu walimuona kama kijana mwema kumbe alikuwa mwenye dhambi.

Immanuel akaendelea kumsikiliza yule mmishonari. "Yesu alivuta umati mkubwa wa watu," alisema, "na walimuona akitenda miujiza. Aliwafundisha hawa wafuasi kuhusu habari za

Mungu. Baada ya muda, watu waliomuonea Yesu wivu walimkamata, wakamsulubisha msalabani na kumuua."

Immanuel alikuwa kwenye hali ya butwaa tena wakati mmishonari akielezea juu ya kifo kibaya cha Yesu. Hatimaye mmishonari alileta habari njema kutoka kwenye simulizi hiyo aliyowapatia.

"Japokuwa mateso ya Yesu yanaonekna kuwa ni mbaya kiasi kile, kilituletea mambo mema. Mungu aliruhusu kwa njia ya kifo cha Yesu Kristo sisi wanadamu tulipiwe deni ya dhambi zetu. Dhambi za kila mmoja wetu," Yule mgeni aliendelea kuweka mkazo. "Ni kama vile baba ambavyo hujitokeza kwa haraka kumnusuru mwanae kipindi ambapo mnyama mkali anakuja kumshambulia, ndivyo ambavyo Yesu aliingilia kati na kupokea hukumu ya kifo kwa ajili yetu. Na kwa sababu ya kile alichokifanya Yesu, dhambi zetu zinafutwa na kutupwa mbali."

Immanuel aliyatafakari maneno haya. Yalikuwa ni maneno ya kweli na yenye kueleweka kwake na akatamani kusikia zaidi. Alijiwazia sababu ya Yesu kutoa uhai wake. Mmishoari alisema ya kwamba Mungu alifanya yote hayo kwasababu Yesu anampenda kila mwanadamu aliyeko duniani.

Kuna sababu nyingine, Immanuel aliendela kutafakari, kuna mtu mwingine anaweza kufanya hivi kwasababu ya upendo tu? Alishangazwa na ukweli ya kwamba baada ya kifo kibaya kiasi kile Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Ili kudhihirisha nguvu yake dhidi ya kifo na mauti. Alijifunza ya kwamba Pasaka ni kusherehekea kuja kwa Yesu, kifo chake kwaajili ya kulipa deni la dhambi, na Yesu kudhihirisha nguvu dhidi ya kifo na mauti.

Yule mmishonari akaendelea kuelezea jambo fulani la ajabu ambalo lilimpelekea Immanuel kuvutiwa zaidi na maneno yake.

"Kila mtu anaye mwamini Yesu na kuchagua kumfuata, siku moja ataenda mbinguni kuishi naye huko. Wale wanaochagua kutomwamini wataenda motoni, sehemu mbaya sana. Ninatoa mwaliko kwa kila mmoja wenu kupokea hii zawadi ya msamaha kutoka kwa Yesu. Huwezi kulipia gharama ya zawadi hii, lakini unaweza kuipokea na kuikubali kama zawadi."

Mara moja Immanuel alikuwa anaihitaji zawadi ile lakini hakuwa anajua ni kwa namna gani anaweza kuipokea. Anaweza kuipokea zawadi hii ya masamaha wa bure?

Mmishonari aliketi chini, na mwalimu aliyekuwa akitafsiri aliendelea kusimama na

kuuliza. “Iwapo kuna maswali yoyote, tafadhali baki baada ya ibada. Utakuja hapa tulipo na tutazungumza nawe wakati wengine watakuwa wakitoka kwenda kuandaa chakula.”

Immanuel alibaki pale alipokuwa wakati watu wengine walipokuwa wakitoka kanisani. Watu wachache walibaki na walisogea mbele kwa utaratibu. Immanuel aliwajua baadhi ya watu hao waliobaki pamoja naye. Alijaribu kumtazama mama yake alipokuwa anageuka ili aondoke kanisani, akiwaita rafiki zake kwa sauti ya juu ili wamsubiri. Immanuel alianza kupiga hatua za kuondoka kumfuata mama yake, lakini mawazo ya moto wa milele yalimrudia. Alibadili mawazo yake mara moja na kugeuka na kuanza kuelekea kule mbele ya kanisa. Kwa sababu fulani, wakati akielekea mbele macho yake yalikuwa yanatazama chini, ardhini tu. Akatembea na kujikuta mbele ya mwalimu wa shule.

“Immanuel, je unataka kumwamini Yesu?”

Immanuel alibaki katika hali ya ukimya, hali macho yake yameelekezwa chini, ardhini.

“Immanuel, kwanini umekuja hapa mbele?”

Kwa mara nyingine tena, Immanuel hakuwa na la kujibu, alikuwa kimya tu. “Mchungaji, tafadhali sogea hapa nakuomba,” Immanuel alimsikia mwalimu akiita.

Yule mchungaji wa kanisa la kijiji, mzee mwenye kipara, aliyevaliza suti na tai nyekundu nyembamba, aliwakaribia na alielewa mara moja.

"Huyu si ndiyo yule kijana anayetokea kule kwenye mwamba ambaye huwa anachunga mifugo?" alimuuliza mwalimu wa shule.

"Ndiyo."

"Kijana," mchungaji alisema, "unapaswa kuomba maombi ya kumpokea Yesu moyoni mwako ili aiokoe roho yako. Je, hiyo ndiyo shauku yako?"

Immanuel alitikisa kichwa.

"Basi unifuatishe namna nitakavyokuongoza. 'Bwana Yesu, mimi ni mwenye dhambi, asante kwa kufa kwaajili yangu, ninachagua kukuamini.'"

Immanuel aliyarudia yale maneno, huku akiyaamini bila kuwa na hali yoyote ya mashaka ndani yake.

"Safi," mchungaji alimwabia. "Sasa unapaswa kuja kanisa kila Jumapili na uanze kuishi maisha yanayomtii Kristo. Tutakubatiza hivi karibuni."

Immanuel alitikisa kichwa chake kwa haraka na kugeuka ili aondoke. Na ghafla alihisi kushikwa na mkono mkubwa begani mwake. Aliponyanyua kichwa alimuona yule mmishonari,

ambaye alimsemesha katika lugha yake ile ya kigeni. Ile sura ya upendo ilimpatia tabasamu. Mmishonari alionekana kufurahia, Immanuel naye alifurahishwa na jambo hili. Jambo lililofuata tu baada ya hapo ni kupatiwa Biblia mikononi mwake. Kwa jinsi alivyomtazama yule mmishonari, Immanul alitambua ya kwamba amepewa ile Biblia kama zawadi.

Immanuel alivuta pumzi kubwa. Alishangaa kupewa kitabu, kiwe kitabu chake mwenyewe, kitabu chenyewe ni Biblia, iliyoandikwa kwa lugha yake!

Katika maisha yake yote Immanuel alishawahi kuona Biblia moja tu, shuleni. Hakuwa anajua mambo mengi sana kuhusu Biblia isipokuwa jambo moja tu ya kwamba Biblia ilikuwa inaeleza habari za Yesu. Alikuwa ni mtu aliyejawa furaha na mwenye shauku kubwa ya kujifunza zaidi juu ya Yesu. Mwili wake ulikuwa mwepesi pindi alipotembea kuelekea nje ya kanisa. Kuna jambo kubwa limetokea kwenye maisha yake—amani imeufunika moyo wake. Alitambua wazi ya kwamba dhambi zake zimesamehewa.

Siku hiyo jioni, yule mmishonari alionyesha "filamu ya Yesu"[1] nje ya jengo la kanisa, kulikuwa na kitambaa kikubwa kilichopachikwa ukutani ili watu waweze kuona filamu kutokea hapo.

Immanuel aliendelea kushangaa zaidi juu ya yale ambayo Yesu ameyafanya na ni kwa namna gani aliwapenda watu.

Wiki iliyofuatia na wiki kadhaa zilizofuatia baada ya hapo Immanuel alifanya kama alivyoagizwa na yule mchungaji mzee. Alihudhuria ibada za kila Jumapili za kanisa. Muda ulivyokuwa ukiendelea, alianza kumtembelea mchungaji nyumbani kwake mara moja kwa wiki ili kujifunza Biblia pamoja. Vijana wengine walijiunga nao. Yule mchungaji mzee alijua habari nyingi sana za Biblia na alikuwa na namna inayovutia ya kuzisimulia.

Hata hivyo, Immanuel alijikuta ni mwenye maswali mengi sana mawazoni mwake. Alijiuliza hizo habari za Biblia zilikuwa na maana gani hasa? Zilikuwa zinahusianaje? Alitamani sana kujua zaidi. Kila mara alifanya mapitio moyoni wake juu ya kile anachokifahamu:

- Yesu ananipenda. Alikufa kwa ajili yangu.
- Dhambi zangu zimesamehewa.
- Yesu ni mwenye uweza.
- Ninaweza kumuomba Mungu na kupokea msaada.
- Mungu ni mwenye uweza wote kuliko shetani, lakini ninapaswa kujitenga mbali na shetani na mbinu zake zote.

- Ninapaswa kumsadia mchungaji na kuwasaidia wale walio kwenye hali ya uhitaji.

Immanuel alijitahidi kuishi katika hali ya utii kwa Yesu Kristo, kama alivyojifunza. Siku zote aliambatana na mchungaji katika kuwatembelea wagonjwa au watu wenye mahitaji kijijini. Alimuona mchungaji akiwaombea. Immanuel aligundua ya kwamba wale watu ambao walitembelewa na mchungaji walimpatia kiasi kidogo cha pesa, kuku, mayai, au vitu vingine ijapokuwa mchungaji hakuwa anawatoza aina yoyote ya malipo!

Immanuel aliendela kujifunza na kukua katika imani. Aliendela kuhudhuria ibada za kanisani na kusoma Biblia yake wakati akichunga wanyama. Miaka miwili baadaye, mchungaji alimuomba Immanuel aanze kuwa anasoma matangazo kanisani kila siku ya ibada. Immanuel alitangaza juu ya ratiba za kanisa na mahitaji ya maombi na maombezi. Alitoa matangazo yanayohusiana na maandalizi ya ujio wa askofu wa kanisa.

Immanuel alianza pia kuitisha sadaka na kugawa mikate na divai wakati wa ibada ya ushirika mtakatifu. Aliendelea kuambatana na mchungaji

wake kutembelea nyumba kadhaa, kuwasaidia na kuwaombea wanakijiji. Lile kanisa dogo likaanza kukua kiidadi. Baada ya yule mmsihonari kulitembelea kanisa, idadi ya watu waliokuwa wakija kwenye ibada iliongezeka maradufu. Hata mama yake Immanuel alianza kuhudhuria kila Jumapili badala ya siku za sikukuu tu. Kisha ghafla, kila kitu kilibadilika tena.

## Maswali—Sura ya Kwanza

1. Immanuel aliishi maisha ya kuridhika katika kuchunga mifugo ya baba yake. Lakini alipokwenda kanisani siku ya Pasaka na kujifunza juu ya habari za Yesu maisha yake na imani yake vilibadilika. Immanuel alitambua wazi ya kwamba anahitaji msamaha wa dhambi zake. Kama ungekuwa umeambatana na Immanuel kanisani siku hiyo, je ungeondoka ibadani au ungeambatana naye kwenda mbele? Kwanini?

2. Je, unayaelewa maombi ambayo Immanuel aliyaomba na mwalimu pamoja na mchungaji? Umeshawahi kufanya maombi ya namna hiyo?

3. Baada ya kuomba msamaha, Immanuel alipata shauku kubwa sana ya kujua zaidi juu ya habari za Yesu. Ili kukidhi njaa yake aliamua kusoma Biblia na kuungana na mchungaji katika kuwahudumia watu wa kijijini kwao. Ni nani ambaye unadhani unaweza kuamabatana naye ili kujifunza zaidi kuhusu Yesu?

# Sura ya Pili:

## Wito wa Kuongoza

Immanuel alienda machungani na kukaa huko kutwa nzima. Wakati wa mchana, jua likiwa linawaka, mama yake Immanuel alikuja huku akiwa analia.

"Mama, ni nini kimetokea?"

Huku akitokwa na machozi, mama yake Immanuel alijibu, "Mchungaji wetu, mzee, amepatwa na mashambulizi. Yupo anaugulia nyumbani kwake…."

Kabla hajamaliza, Immanuel alinyanyuka na kuanza kukimbia kwa kasi, miguu yake mikubwa ndiyo ilikuwa msaada wake kuelekea kwenye nyumba ya mchungaji. Alipokuwa akifika, alikutana na mwanakijiji mmoja mlangoni. "Pole," yule mwanakijiji alimwambia Immanuel. "Mchungaji wetu amefariki dunia. Tumetuma ujumbe ili askofu aje kutusaidia. Lakini nawe unapaswa kusema kitu kwenye msiba huu." Immanuel alijisikia hali ya uzito mkubwa moyoni mwake wakati akitembea kurudi machungani.

Siku iliyofuatia wazee wawili wenye umri mkubwa kutoka kanisani walimfuata nyumbani

kwao na kumwambia. "Iwapo askofu ataridhia, unapaswa uchukue nafasi kama mchungaji mpya. Sisi tumekwisha kukubaliana, na washirika wa kanisa wamekubaliana na maamuzi hayo." Immanuel alikuwa makini kuwasikiliza wakati wakiendelea kuzungumza.

"Wewe una ujuzi mzuri zaidi wa kusoma Biblia pale kanisani. Umekuwa mwaminifu na mtiifu tangu umemwamini Yesu. Unajua namna ya kuwatembelea watu na kuwoambea."

Wazee wakatulia hali wakimtazama Immanuel kwa umakini. "Watu wote wanakubaliana na hili. Mungu ameweka wito wa kumtumikia kwenye maisha yako."

Immanuel akaondoka kwenda kuchunga mifugo ya baba yake, huku mambo mengi yakiwa yanaendelea kwenye mawazo yake. Aliyarudia maneno ya wale wazee mara nyingi iwezekanavyo, na kuanza kuona jinsi maisha yake yatakavyobadilika.

Siku ya ibada ya maziko Immanuel alisoma Biblia na kuhubiri maneno mafupi tu. Hakupata ugumu wowote kufanya hivyo. Japokuwa askofu alihubiri kwa kirefu, Immanuel yeye aliongea kwa kifupi kisha akaomba, akimshukuru Mungu kwaajili ya zawadi ya maisha ya mchungaji wao.

Baada ya ile ibada Immanuel alikuwa na shauku ya kumuuliza askofu juu ya nini cha kufanya, lakini alikuwa na hali ya uoga. Mawazoni mwake kulikuwa na maswali mengi sana yanaendeea hasa pale anapokumbuka ya kwamba Jumapili itawadia ndani ya siku tatu zijazo. Je, afanye nini Jumapili hiyo? Je, aseme nini siku hiyo? Immanuel alikuwa na mashaka. Anaweza kuchukua nafasi ya mchungaji wake? Mchungaji wake amekaa kwenye nafasi na kazi hii kwa miaka mingi na aliifanya kazi hii kwa uzuri.

Immanuel aliyatafakari pia maisha yake kwa namna hiyo. Alikuwa anajua kusoma, alikuwa anajua kuchunga mifugo ya baba yake, na anajua kwa kiasi kuhusu maisha ya mchungaji wake kwa kuishi naye kwa ukaribu na kutenda naye kazi ya huduma. Maswali ya kina yalimzonga wakati wote. Hivi hali huwa inakuwaje pindi mtu anapobeba jukumu la kuchunga kanisa la Mungu? Mtu anawezaje kuwa mwalimu na kiongozi mzuri? Maisha yake yanapaswa kuwa na mwonekanao gani kwenye nafasi na jukumu hili jipya la kichungaji; na ni nini hasa maana ya kuwa mchungaji?

Immanuel alikuwa amejawa na maswali mengi sana kuliko majibu. Hofu zake ziliinuka, na akawa katika hali ya kujiuliza iwapo anaweza

kufanya kazi ambayo wazee wamemuomba afanye. Kwa kweli mtu mwingine anapaswa kubeba jukumu la kulea kanisa hili.

Lakini hakuna mtu mwingine aliyejitokeza. Askofu alipokuwa amekaribia kuondoka kijiji hapo, alimtembelea Immanuel na kuthibitisha maamuzi ya kanisa. "Unapaswa kuchukua mambo uliyojifunza kutoka kwa mchungaji wako mzee na kuyatenda. Ikimpendeza Bwana, nitarejea hapa baada ya muda wa majuma kadhaa ili kuona uanendelaje."

Askofu alimfundisha Immanuel mambo kadhaa ya kiutendaji kama vile namna ya kuweka fedha za kanisa kwenye akaunti ya benki ya kanisa. Immanuel alisikiliza, lakini bado alikuwa mwenye hofu juu ya kwenda kwenye lile kanisa dogo kama mchungaji wa kundi la Bwana kwenye kijiji.

"Lakini askofu," Immanuel alionyesha hali ya kusita. "Nifanye nini siku ya Jumapili? Niseme nini?"

Askofu alimwangalia Immanuel kwa hali ya upendo. "Fanya vile ambavyo mchungaji wako alikuwa akifanya, na utafanikiwa. Nitakuombea."

Siku ya Jumapili ikawadia na Immanuel akajikuta mbele ya umati wa kanisa akihangaika, wakati askofu amekaa kwenye benchi mbele

yake. Washirika wengi wa kanisa walikuwa wenye majonzi juu ya kuondokewa na mchungaji wao mpendwa. Immanuel aliungana nao. Alisoma neno kutoka kwenye Biblia kisha akawaombea watu. Alimshukuru Mungu juu ya ahadi yake ya mbingu. Waongozaji wa nyimbo waliliongoza kanisa katika kuimba nyimbo za mapambio ya kumimina mioyo yao kwa Mungu.

Immanuel alijisikia kupata hali ya pumziko ndani yake. Ameweza. Askofu alizungumza naye wakati anajiandaa kuondoka, kumpa maoni ya nyongeza.

"Immanuel," alisema, "Kwenye kijiji kikubwa cha jirani utapata madarasa maalum kwaajili ya viongozi wa kanisa kama wewe, ambayo hufundishwa na mwalimu mzoefu mwenye elimu kutoka chuo cha Biblia."

Wale wazee wawili waliomfuata Immanuel nyumbani kipindi kile cha msiba na kumuomba aongoze kanisa waliafikiana na maneno ya askofu na kumwambia Immanuel ni wapi madarasa hayo yako. Immanuel alijua wazi ya kwamba anaweza kuendesha baiskeli yake takriban kilometa ishirini kwenda na kurudi kwenye madarasa. Njia ya kuelekea huko ilikuwa ni kupitia barabara ya vumbi inayotoka kijijini kwao kisha inaungana na barabara

kuu ambalo lililkuwa linaelekea kwenye kijiji kikubwa. Alipangilia utaratibu wa namna gani ndugu zake watashughulikia mifugo ya baba yake siku za Jumatatu ili yeye apate muda wa kuhudhuria mafunzo.

Immanuel alionekana mwenye furaha juu ya nafasi hii ya kujifunza namna ya kuchunga kanisa la Mungu. Kama Mungu amemwita, huenda sasa Mungu ataonyesha ni namna gani anapaswa kutimiliza majukumu ya wajibu wake mpya.

## Sura ya Pili: Maswali

1. Kuna nyakati Mungu anaruhusu mambo fulani yatokee ambayo yanayabadilisha maisha yetu kabisa. Immanuel alikutana na badiliko hili baada ya mchungaji wake kufa, na akapokea wito wa kuongoza. Je, umekutana na hali ya namna hii? Je, uliipokeaje?

2. Immanuel alijisikia hali ya woga alipoombwa kuongoza kanisa. Alikuwa na maswali mengi kuliko majibu. Huwa unafanya nini pindi unapogundua ya kwamba maisha yako yanabadilika na unakuwa na hali ya woga?

3. Immanuel aliona ya kwamba Mungu huachilia majawabu. Mungu alimwelekeza afanye jambo fulani jipya, lakini pia alimwandalia mahala pa kujifunza kutimiliza jukumu hili jipya. Ni lini ulimwamini Mungu kukuwezesha kuchukua jukumu jipya na usilolitarajia?

# Sura ya Tatu:

## Utambulisho Mpya

Immanuel aliendesha baiskeli yake kwa shauku kuelekea kwenye kijiji kile kikubwa, huku akijiuliza itakuwaje pindi atakapoanza kujifunza chini ya mwalimu mwenye elimu ya Biblia. Ndipo akatokeza mbele ya jengo lenye ukuta usio na maandishi yoyote, chumba cha darasa kisichotumika, kilichoandaliwa maalum kwaajili ya madarasa husika. Immanuel alijichagulia mahali pa kuketi kwenye dawati moja la muda mrefu, kisha akaipenyeza miguu yake chini ya dawati. Aligundua kuna wanafunzi tisa kwa ujumla wao, kama yeye, wamewasili kutoka vijiji mbalimbali, na kisha mwalimu alisimama mbele yao.

Immanuel alichomoa Biblia yake na kuiweka juu ya dawati, alifurahi kwamba hakuisahau. Akagundua ya kwamba wanafunzi wenzake walibeba Biblia zao pia.

"Karibuni. Bwana ni mwema, wakati wote. Wakati wote, Bwana ni mwema!"

Salamu ya mwalimu wa darasa aliachilia hali ya tabasamu kwenye uso wa Immanuel. Alinyofoa kipande cha karatasi kutoka kwenye

Biblia yake na penseli kutokea kwenye mfuko wake. Kimsingi alikuwa amepania kutopoteza jambo lolote ambalo anapaswa kujifunza siku hiyo.

"Somo letu litajikita katika kutambua shughuli za mchungaji katika kanisa la Mungu. Ni kitu gani hasa mchungaji anapaswa kufanya?"

Immanuel alinyofoa penseli yake na kuiweka tayari akiwa katika hali ya matarajio. Huenda somo hili likajibu maswali aliyonayo moyoni mwake!

"Fungueni Biblia zenu kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume, sura ya 20," mwalimu wa somo aliwaambia. Alishikilia Biblia yake. "Tutajifunza kutoka kwenye Biblia, Neno la Mungu. Hatupaswi kujielekeza kwenye mitazamo ya wanadamu au dunia inayotuzunguka inasema nini. Kama wachungaji wa kanisa la Mungu tunapaswa kufuata neno la Mungu pekee. Tutajifunza Kutokea humo na si kwingineko."

Mwalimu aliiweka Biblia yake kwenye mimbari. "Watu wengi, pamoja na viongozi na wachungaji, hawaifuatilii Biblia kwa ukaribu na umakini kama inawavyowapasa. Iwapo tutasikiliza sauti nyingi sana, tutachanganywa tu. Ni lazima tujikite kwenye kile ambacho Biblia inasema ili mawazo yetu yawe sawa."

Immanuel akaanza kupekua kurasa za Biblia yake kwa hali mpya ya heshima. Zaidi ya siku zote, sasa alikuwa na kiu kuyaelewa maneno ndani ya kitabu hiki.

“Hebu tuzungumze kuhusu viongozi wa kanisa na jinsi ambavyo wamekuwa wakiitwa majina tofauti tofauti na watu. Umekuja kwenye darasa hili kwasababu unaongoza kanisa. Kuna watu watakutazama na kuanza kukuita mchungaji au mwinjilisti pia kuna wengine wanaweza kukuita kiongozi wa kanisa, askofu, au mzee. Unaweza kuyasikia majina mengine pia.” Mwalimu aliigusa tena Biblia yake. “Lakini sehemu ya lugha kwenye lugha ya asili ya Agano Jipya, kuna maneno mitatu yanatumika kumwelezea kiongozi wa kanisa la mahala pamoja. Tunayaona maneno yote hayo matatu kwenye Matendo ya Mitume sura ya 20. Kila neno linatueleza namna tofauti za kulea kanisa.”

## Mzee ni nani?

Immanuel alikuwa akimfuatilia mwalimu kwa ukaribu sana kwa kusoma Matendo ya Mitume 20:17.

“‘Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa.’ Mtume Paulo, alipokuwa akisafiri, alitaka kuwaita kwa pamoja

viongozi wa kanisa. Hapa anawatambulisha kama wazee wa kanisa. Neno hili linamaanisha watu wakomavu—wenye uzoefu wa kimaisha. Haimaanishi sana swala la umri, kwasababu kuna wazee kiumri ambao hawaonyeshi ukomavu wowote kwa jinsi wanavyoyaishi maisha yao kama sote tujuavyo."

Immanuel na wanafunzi wenzake walicheka kidogo. Alijisikia ahueni baada ya kugundua ya kwamba neno hili halikumaanisha umri kwasababu yeye mwenyewe si mtu wa umri mkubwa.

"Vijana kama Timotheo, walitumika kwenye nafasi ya uzee wa kanisa. Tunasoma habari zao kwenye Agano Jipya. Neno mzee linatumika kumaanisha mtu ambaye anaonekana kuwa mkubwa na mwenye hekima hata kama ana umri mdogo. Mchungaji wa kundi la Mungu anapaswa kuonyesha ukomavu na hekima haijalishi ana umri gani. Ili watu waweze kumtazama na kumwendea wapate kujifunza kutoka kwake."

Immanuel alianza kujihoji iwapo anakidhi kwenye hivyo vigezo. Hakuwa na uzoefu mwingi wa kutosha hata hivyo. Aliendelea kumsikiliza mwalimu alipoendelea kufundisha neno jingine linaloeleza juu ya viongozi wa kanisa.

## Mwangalizi ni nani?

Mwalimu akasoma Matendo ya Mitume 20:28. "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe."

Mwalimu aliinua kichwa juu na kutazama. "Paulo anazungumza na watu walewale ambao aliwakusanya kwenye mstari wa 17, lakini sasa hivi anawaita waangalizi badala ya wazee. Neno waangalizi linamaanisha kile linachokisema. Waangalizi huangalia utendaji wa shughuli na huduma zinazoendelea ndani ya kanisa. Wanawajibika juu ya yale yanayoendelea ndani ya kanisa, kama vile kuweka mipango, maamuzi ya namna gani ya kufanya utumishi ndani ya kanisa, kuratibu namna ambavyo fedha ya kanisa inatumika, na kuchagua mafundisho yanayopaswa kufundishwa ndani ya kanisa."

Mwalimu alipiga hatua kuulekea ubao uliokuwa nyuma yake na kisha akaandika Orodha. "Orodha hii inawakilisha baadhi ya majukumu kati ya mengi ambayo Agano Jipya linayataja kuhusiana na waangalizi wa kanisa."

Immanuel akainakili ile orodha kwa umakini sana. Alinukuu maandiko yote yaliyoam-

batanishwa na mwalimu ili aweze kuyarejelea pindi arudipo kijijini kwao:

- Kuwa na maoni juu ya mafundisho sahihi na maisha ya mkristo yanavyopaswa kuwa (Matendo ya Mitume 15:2-22).
- Kuwa mawakili wema wa fedha ya kanisa (Matendo ya Mitume 11:29-30).
- Kuwaongoza na kuwasimamia watu wanaotumika ndani ya kanisa (Matendo ya Mitume 15:22; 21:18).
- Kufundisha neno la Mungu kwa watu (1 Timotheo 5:17).
- Kulilinda kanisa dhidi upotofu na mafundisho ya uongo (Matendo ya Mitume 20:29-31).
- Kuombea wagonjwa (Yakobo 5:14).
- Kuonyesha kielelezo cha kiungu mbele wa kundi (1 Petro 5:3).
- Kutumika kwa unyenyekevu pamoja na watumishi wengine ndani ya kanisa (Matendo ya Mitume 14:23; 1 Petro 5:1-3).
- Kupata heshima ya kundi wanaloliongoza (1 Wathesalonike 5:12-13; Waebrania 13:7, 17).

Mwalimu aliligeukia darasa lake. "Tunaona kwa uwazi kabisa kutoka kwenye Agano Jipya ya kwamba kutumika kama mwanagalizi wa

kanisa ni jukumu la muhimu sana. Jukumu hili linajumuisha kuangalia hali ya kundi. Hebu sikiliza kile ambacho Waebrania 13:17. 'Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana hao wanakesha kwaajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu…'"

"Sasa sikilizeni kile ambacho Yakobo 3:1 inasema. 'Ndugu zangu, msiwe waalimu wengi, mkijua ya kwamba tutapata hukumu kubwa zaidi.' Hii ni angalizo la kulichunga kundi la Mungu kwa umakini na uangalifu mkubwa!"

Mwalimu alikaa kitako kwenye kiti huku akiwatazama wanafunzi. "Tunaweza kusema ya kwamba viongozi wa kanisa, kama ninyi mlivyo, wanafanya kazi kama makamu-wachungaji, ambao wanatumika chini ya Bwana Yesu. Bwana Yesu pekee ndiye Mchungaji Mkuu. Kama walivyo wakuu wote, siku moja Mchungaji Mkuu atakagua kazi ya kila mmoja anayetenda kazi chini yake. Biblia inatukumbusha wazi ya kwamba Yesu Kristo ndiye aliyemnunua kila mmoja aliye chini ya uangalizi wetu kwa damu yake mwenyewe, ambayo aliimwaga msalabani. Mnakumbuka Matendo ya Mitume 8:28? Mwisho wa andiko hili unafunua ukweli huu. Yesu alilinunua kundi la Mungu kwa bei kubwa na analijali sana. Hivyo tunapaswa kufanya vivyo hivyo."

Immanuel alijisikia hali ya kuhuishwa kwa upya tena. Akaiambia akili yake ya kwamba anapaswa kukesha, kulitunza kundi la Mungu alilopewa.

"Hatupaswi kutumika ili kujipatia malipo ya kifedha au ujira wa namna yoyote ile," Mwalimu alifafanua. "Usidiriki kuongoza kwa lengo la kutawala kimabavu, badala yake ongoza kama kielelezo kwa kundi. Waelekeze kwa upole, ukilisimamia na kulilea kanisa katika njia ipaswayo. Hebu tutazame mistari mingine ya nyongeza."

Immanuel aliendelea kuambatana na mwalimu wa Biblia alipokuwa akisoma:

> Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya kielelezo kwa lile kundi. Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka. (1 Petro 5:2-4)

> Wazee watawalao vema wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha. (1 Timotheo 5:17)

“Japokuwa kazi hii imeambatana na majukumu makubwa na mazito, Bwana Yesu anaahidi kuwazawadia thawabu kubwa wale watendao kazi hii, siku moja atawapatia viongozi ‘taji ya utukufu, ile isiyokauka’ (1 Petro 5:4) atakaporejea.”

Mwalimu alisimama juu, hali akiwa ameshiklia Biblia yake. “Kumbuka, Bwana Yesu Kristo analipenda kundi lake kwa upendo wa kipekee na anawathamini wale ambao wanalichunga na kulitunza kwa umakini. Yesu alimuuelekeza Mtume Petro mara tatu juu ya, ‘chunga kondoo zangu’ (Yohana 21:15-17.) Tunapaswa kutafuta kumpendeza Yesu katika kazi zetu na si kujitafutia ridhiko letu binafsi.”

Mwalimu alitabasamu. “Tumejifunza mengi mpaka hapa kwa leo. Tupate mapumziko mafupi.”

Mawazo ya Immanuel yalikuwa yakikimbia huku na kule wakati ameketi akifanya mapitio ya yale aliyoyaandika kutokea kwenye mafundisho ya mwalimu. Hajawahi kusikia aina hii ya Mafundisho hapo kabla. Alianza kujihoji iwapo kijana mdogo kama yeye anaweza kuyatimiliza yote hayo. Immanuel alimkumbuka mchungaji wake, yule mzee. Alianza kubainisha ni kwa namna gani mzee huyo aliyaishi mafundisho

yake kwa sehemu kubwa kama yalivyofafanuliwa na mwalimu:

- Aliishi katika hali ya upole.
- Hakujitafutia kuvuna fedha kutoka kwa watu.
- Aliwakemea kwa nguvu wale waliokuwa wakiishi katika hali ya dhambi au kufundisha uongo.
- Alikuwa ni mtu jasiri, lakini mnyenyekevu.

Immanuel alikumbuka wakati mmoja ambapo yule mchungaji alimkea mshirika mmoja wa hapo kijijini kwasababu ya maisha ya dhambi aliyokuwa akiyaishi. Alikumbuka waziwazi namna ambavyo alijisikia aibu na fedheha kwa namna ambapo mchungaji aliikabili dhambi ndani ya yule mpendwa bila kupindisha kweli. Sasa Immanuel alianza kuelewa. Alitambua ya kwamba mchungaji wake alikuwa anapambana kutimiliza wajibu wake kama mchungaji, kuyaishi na kuyafundisha mafundisho ya kweli ya imani ya Kristo katika hali ya usahihi wote, na alijipatia heshima miongoni mwa jamii. Immanuel alianza kujisikitikia kwa kuwa alifanya makosa kusikia aibu na fedheha wakati mchungaji wake anakabiliana na ile hali ya maisha ya dhambi.

Immanuel aliweka chini daftari lake na kuanza kupiga funda la chai yake.  Hali ya kutiwa moyo ilianza kufurika ndani ya moyo wake. Maono ya namna gani ya kutenda kazi kama mchungaji wa kanisa la Mungu yalianza kujengeka ndani ya moyo wake. Alitaka kujifunza zaidi. Wakati anamalizia kikombe chake cha chai alirudi kwenye dawati lake na kufungua daftari lake kwenye karatasi ambayo haijaandikwa neno lolote bado.

## Mchungaji ni nani?

Wanafunzi wengine walimaliza na kurejea darasani na Immanuel aliisikia ile hali ya matarajio ya moyo iliyokuwa ndani ya kila mmoja wao na ilikuwa imekijaza chumba kile cha darasa. Alimshukuru Mungu kimya kimya kwa kuwa miongoni mwa watu waliopata neema kukaa kwenye darasa la mwalimu huyo.

"Niliwaahidi kuwafundisha maneno matatu yanayotumika kuelezea kazi ya mchungaji ndani ya kanisa. Tumeshazungumzia mawili tayari, mzee na mwangalizi. Neno la tatu ni neno ambalo tumelitumia karibia siku nzima ya leo—mchungaji. Tumeliona hili neno kwenye Matendo ya Mitume 20:28. Neno hili linaelezea aina ya huduma ambayo viongozi wa kanisa

la mahala pamoja hufanya kwa watu wao. Huwachunga watu wao. Kimsingi neno hili linatokana na wale watu wanaoangalia mifugo, kitu ambacho kipo ulimwenguni mwote."

Immanuel alijitabasamia mwenyewe. Kwamba hiki ni kitu ambacho na yeye anakijua, kwakuwa amechunga mifugo ya baba yake kwa kipindi kirefu!

"Mchungaji husimama katikati ya kundi lake na kuliongoza," mwalimu alisema. "Mchungaji hulifundisha kundi lake. Hulilinda dhidhi ya mashambulio ya aina yoyote ile. Hii ndiyo sababu niliyoisema hapo awali ya kwamba kiongozi wa kanisa anapaswa kutoa muda wake katika kula neno la Mungu. Sote tunapaswa kujifunza na kufundisha, na kisha kuhubiria kundi ambalo Mungu ametupatia. Hebu tusome maandiko kadhaa pamoja."

> Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu. (Waefeso 4:11)

> Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. (2 Timotheo 2:15)

"Maandiko haya yanatusababisha tuelewe ya kwamba kuchunga kanisa na kulifundisha si kuamka Jumapili asubuhi na kuanza kusema chochote kitakachokuijia mawazoni mwako. Hapana, si hivyo hata kidogo!" mwalimu aliweka mkazo. "Wekeza muda kujifunza na kuhakikisha uelewa wako uko sawa, ili uweze kuwafundisha watu kitu fulani maalum kila wiki kutokea kwenye kweli ya neno la Mungu. Wachungaji ni watu ambao wamejitoa katika kujifunza, kusoma, kupata maarifa, na kufundisha."

"Mnakumbuka niliwaambia kuhusu kiongozi mmoja wa kanisa aliyekuwa na umri mdogo kwenye Agano Jipya aliyekuwa anaitwa Timotheo? Mtume Paulo anampatia jambo zuri la kukumbuka katika mstari ambao tumeusoma. Paulo anamwambia 'kutumia kwa halali neno la kweli' (2 Timotheo 2:15). Jambo hili linapaswa kuwa endelevu miaka yetu yote. Tunajifunza neno la Mungu ambalo linatuandaa kufundisha kila wiki. Ni mara nyingi tunaona viongozi wa makanisa ya mahala pamoja wakijidhabihu katika kujipatia maarifa zaidi na kujifunza kwingi, kama ilivyo kwa wengi wetu walivyojidhabihu kufika hapa leo. Usisahau umuhimu wa kufundisha ukweli tena kwa bidii. Hii ni sehemu kubwa ya kazi ya kulichunga kanisa la Mungu."

Mwalimu aliruhusu muda wa maswali na mjadala walipofika mwisho wa kipindi. Kabla wanafunzi hawajatawanyika kwaajili ya wiki iliyokuwa mbele yao, mwalimu aligeukia ubaoni kwa mara nyingine tena. "Mnakuumbuka kile tulichojifunza kwenye yale majina matatu ambayo wanaitwa viongozi wa kanisa?" Aliuliza huku chaki yake akitembea kwenye ubao.

- Cheo tunachopewa na watu si kitu cha muhimu. Tunayoyafanya Kutokea kwenye cheo hicho ni ya muhimu zaidi.
- Kiongozi hutenda kama mzee, kwa ukomavu na hekima. Huwashauri watu vyema kiasi kwamba wale walioko kanisani humuheshimu na kumwamini.
- Kiongozi hutenda kama mwangalizi, hupangilia majukumu muhimu ya kanisa na kuliongoza kanisa huku akiongozwa na hali ya maombi.
- Kiongozi hutenda kama mchungaji. Hufundisha, hutunza na kuongoza kundi.

Mwalimu alitua chaki yake chini kisha akaligeukia darasa lake. "Jambo moja zaidi, ambalo inawezekana mmeshaliona kutoka kwenye maandiko tuliyoyasoma hivi leo. Kila kanisa linapaswa kuwa na viongozi

kadhaa. Hauongozi kanisa ukiwa peke yako. Mnakumbuka Matendo ya Mitume sura ya 20 ambapo Mtume Paulo aliwaita kwa pamoja 'wazee,' wingi, si mzee mmoja? Mtume Paulo alipochagua wazee kama tusomavyo kwenye Mtaendo ya Mitume 14:23, aliteuwa 'wazee' kwa kila kanisa, si mzee mmoja tu. Hii kazi ni kubwa sana kiasi kwamba mtu mmoja hatoshi."

Mwanafunzi mmoja alinyoosha mkono. "Mwalimu, mimi nipo peke yangu tu pale kanisani kwetu. Hakuna watu waliojitokeza mbele kuja kuungana nami kuongoza kanisa."

"Ndiyo," alijibu mwalimu. "Nyakati hizi hutokea. Jitahidi kwa kuwekeza muda kufinyanga wengine kwa haraka iwezekanavyo kisha uwaweke kwenye nafasi za kiuongozi mara tu baada ya kuwa wameelewa namna ya kuongoza. Wachungaji huongoza kundi, lakini pia hufinyanga viongozi wengine."

Sasa Immanuel akaendelea kuelewa kwanini mchungaji wake alikutana naye na kujifunza Biblia kwa pamoja, kwanini alimchukua na kuambatana naye kwenye kutembelea washirika, na kwanini alimkabidhi majukumu siku ya Jumapili. Aliwekeza muda kumuandaa Immanuel kwaajili ya uongozi!

Immanuel, hali akiwa ametiwa moyo na maswali ya wanafunzi wenzake, akajisikia huru kuuliza swali lake. “Mwalimu, mchungaji wangu, yule mzee aliyefariki, alinichukua ili niambatane naye katika kuwatembelea watu. Alisoma Biblia pamoja nami na alifundisha maswala ya uongozi. Lakini washirika wangu wanadhani ya kwamba ninapaswa kufanya kila jambo mimi mwenyewe. Nifanye katika hilo?”

“Kwa sasa unaweza ukaliacha jambo hilo kwa muda.” Mwalimu alijiegemeza kwenye mimbari ya darasa. “Lakini hebu fikiria hivi. Mchungaji wako, yule mzee, alifanya jambo jema kama inavyotakiwa kukufinyanga wewe kuwa kiongozi. Alitambua wazi ya kwamba jukumu hili ni kubwa kiasi kwamba haliwezi kufanywa na mtu mmoja. Kwa kadiri kanisa linavyozidi kukua, ndivyo tunavyohitaji viongozi wengi kusaidia. Hatuwezi kujilimbikizia majukumu yote sisi wenyewe binafsi kwasababu ya wivu. Kuandaa viongozi wengine husababisha ustawi wa huduma.”

Mwalimu aliwatazama wanafunzi wake wote. “Hakuna kiongozi ambaye atatimiliza yote bila kukosea kama alivyokuwa Bwana wetu Yesu Kristo. Sisi, wanadamu, tuna ukomo wetu katika utendaji. Iwapo viongozi watakuwa katika hali

ya umoja, wataonyesha kilelezo kizuri cha umoja ambao Mungu anapenda kuuona ndani ya watu wake na kanisa lote kwa pamoja litakuwa imara."

Mwalimu alichagiza. "Ninaamini mmewahi kusikia usemi mmoja usemao 'vichwa viwili ni bora kuliko kimoja.' Hatujawahi kuwaona watu wanatembea huku mtaani wakiwa na vichwa viwili, lakini tunajua ya kuwa zaidi ya akili moja ikitumika kulitazama jambo moja kutakuwa na hekima namna ya kuliendea. Ndiyo, ni vyema kuwa na kiongozi zaidi ya mmoja. Unapofanya hivyo, mnashauriana, mnatiana moyo, na kusaidiana katika kazi yenu."

Sasa mwalimu akajielekeza tena kwa Immanuel. "Kwahiyo, tenda kama mchungaji wako alivyotenda. Tafuta watu ambao wanaweza kuwa viongozi. Wafinyange."

"Neno moja la mwisho kwa darasa," mwalimu alisema. "Kumbukeni, tuna Mchungaji Mkuu mmoja, Yesu. Anawaita wengi waje kutumika kama makamu-wachungaji. Kazi yetu inabaki pale pale kuwaelekeza watu kwa Mchungaji wao Mkuu, Mwokozi na Mkombozi wetu, haijalishi tunafanya nini au ni viongozi wangapi tumefinyanga."

Baada ya darasa, Immanuel alijisogeza kwenye baiskeli yake na kuanza kuendesha.

Alijisikia mwenye furaha isiyomithilika! Hakujali sana hali ya mazingira yake hata alipoingia kwenye barabara nyembamba, yenye mabonde na vumbi iliyokuwa inaelekea kijijini kwao. Hakutambua hata idadi ya ng'ombe na mbuzi aliokuwa akiwavuka kwenye makundi ya mifugo kinyume na ilivyokuwa desturi yake. Mawazo yake yalikuwa yamezama na kupotelea kwenye mafundisho aliyoyapokea darasani.

Japokuwa alikuwa amejawa na furaha isiyopimika lakini alikuwa na wingi wa shukurani kwa kupata mwongozo. Sasa ufahamu wake juu ya kazi ya uchungaji uliongezeka. Alimuomba Mungu ili aweze kutimiliza kazi yake inavyotakiwa. Immanuel aliutazama umri mdogo aliokuwa nao lakini aliendelea kushikilia ule wito ambao Mungu amempa kuutimiliza. Alijikuta akitamani Jumatatu inayofuata ifike haraka na aliendelea kufikiria ni kwa namna gani atafundisha siku ya Jumapili kanisani kwake juu kile alichojifunza kwenye darasa la leo. Ili washirika wake wajifunze pamoja naye.

# Sura ya Tatu: Maswali

1. Mchungaji wa Immanuel alipofariki, Immanuel aliitwa ili kubeba jukumu hilo la kichungaji. Wazee wawili kutoka kanisani kwao walimuomba achukue nafasi ya mchungaji wao kwasababu waliona ya kwamba ana maisha ya uaminifu. Je, unadhani wangeweza kusema hivyo juu ya maisha yako? Kama sivyo, ni jambo gani unahitaji kulishughulikia?

2. Kwanini uaminifu ni wa muhimu kuliko karama na vipaji?

3. Immanuel alichangamkia nafasi ya kujifunza namna ya kuongoza kanisa. Ni kwa namna gani wewe unaweza kujifunza juu ya Mungu na namna ya kulichunga kanisa la Mungu?

4. Immanuel alidhihirisha huruma kubwa kwaajili ya watu wa kanisani kwao ambao walimkosa mchungaji wao wa zamani. Ni kwa namna gani aliwatia moyo? Je, huwa unawatia moyo kwa namana gani wale wanaokuja kwako katika hali ya huzuni?

5. Mwalimu wa darasa la Jumatatu alisema ya kwamba maandiko yamewapa viongozi wa kanisa majina mitatu. Taja majina hayo. Mwalimu alisema ni kitu gani ni cha muhimu zaidi kuliko cheo, jina au wadhifa?

6. Je kuna watu ambao wanaweza kuwa viongozi na unawaona kanisa kwako? Ni nani unaweza kuanza kumfundisha kama sehemu ya kumuandaa kuwa kiongozi?

# Sura ya Nne:

## Rafiki Mpya

Immanuel alijitupia tena kwenye barabara yao ya vumbi, huku kichwani akianza kuwaza juu ya kile atakachojifunza tena kwenye siku yake ya pili kwenye. Aliingia kwenye chumba cha darasa ambacho hakikuwa kigeni kwa sasa na kukaa kwenye kiti kilekile alichokalia wiki iliyopita. Wanafunzi wenzake nao waliingia na kila mmoja kuchukua nafasi yake.

"Habari yako kijana?" Immanuel aligeuka ili aweze kutazama mwenye sauti ya kutetemesha hivyo ni nani. Akakutanisha macho na mwanaume mmoja mwenye umbo kubwa, sura ya duara na kitambi kikubwa ambaye alikuwa ameketi pembeni yake.

"Unaitwa Immanuel, si ndiyo?"

"Ndiyo."

"Ndiyo," yule mwanaume mwenye sura ya duara alirudia jibu la Imaanuel huku akimwangalia kutokea juu mpaka chini. "Ninakijua kijiji chako. Niliwahi kutembelea huko wakati mmoja, miaka mingi, mingi iliyopita. Nimewahi kukutana na

mchungaji wako, yule mzee. Ninajua ni pigo kubwa yeye kuondoka duniani."

"Ndiyo," Immanuel alijibu kwa hisia kali za moyo.

"Na," yule mwanaume alaiendelea kusema, "Wewe ulichukua nafasi yake kama mchungaji mpya?"

"Ndiyo."

"Sawa," yule mwanaume alijibu kwa sauti nzito. "Hilo ni jambo jema sana kwako, na umefanya vyema sana kuhudhuria madarasa haya. Mwalimua anayefundisha ninamfahamu vyema. Ni mtumishi mzuri sana wa Mungu."

Immanuel alijisikia kutiwa moyo na huru kuzungumza kutokana na ukarimu wa huyu mtu mgeni kwake. "Umekuwa mchungaji kwa muda gani?" aliuliza Immanuel.

"Oh," jibu lilikuja. "Kwa muda mrefu sasa. Nimechunga kwenye kanisa kule mjini kati kwa miaka ishirini na nne sasa. Nikaenda kwenye chuo kimoja cha Biblia huko na sikuweza kuondoka kutoka huko." Yule ndugu akajitengeneza kwenye kiti chake ili awe huru kiasi. "Mimi na marafiki zangu tulianzisha kanisa tukiwa na watu kumi na mbili; tunaendelea kukusanyika hata kwenye ibada zenye mahudhurio ya watu mamia."

Immanuel alionyesha hali ya mshangao. “Umesoma chuo cha Biblia?”

“Ndiyo, kwa miaka mitatu.”

“Sasa, kwanini unakuja kwenye madarasa ya namna hii?”

“Ha, ha, ha!” Kicheko cha furaha kilitiririka kutokea ndani ya tumbo la huyu mwanaume. Ni mtu ambaye amejawa na furaha muda wote.

“Sasa, kijana wangu, hebu acha nikudokeze hili. Nimetambua ndani ya miaka hii yote ya kwamba ninapaswa kujifunza. Ninatafuta sehemu mbalimbali za kujifunza. Iwapo nitaona fursa kwenye kongamano, darasa maalum, semina, au kusanyiko lolote ambalo lipo kwa wakati huo, ninahudhuria.”

Immanuel aliendelea kushangaa umbali ambao ndugu huyu amesafiri, akajaribu kuwazia changamoto za kwenda huku na huko ili tu kujifunza. Akajiuliza laiti ingelikuwa ni yeye angeendesha baiskeli kwa muda kiasi gani?

Ile sauti nzito iliendelea kuongea. “Kanisa langu limekuwa kubwa sana na Bwana akafungua mlango wa kupata usafiri wa gari. Kwa sasa ninaweza kwenda sehemu mbalimbali. Nimeambatana na wachungaji wawili kutoka kwenye dhehebu letu kuja nao kwenye madarasa haya leo.”

Yule mwanaume akachukua penseli yake na kunyoosha karatasi yake. “Sote tunahitaji kujifunza, na nimegundua jambo moja Immanuel, ya kwamba hata kama hakuna jambo jipya kabisa la kujifunza kwa wakati huo huwa ninapaswa kujikumbusha mambo ambayo inawezekana nilipitiwa, sikuyaelewa darasani. Kwa mfano, wiki iliyopita, mwalimu alikazia umuhimu wa kujifunza neno la Mungu ili tuweze kulifundisha. Nilihitaji kukumbushwa hivyo. Kuna nyakati ninajikuta nimetingwa na mambo mengine—mambo mazuri na mema kabisa—kama vile kufanya mikutano, huduma ya yatima, au kukusanya fedha kwaajili ya kuwahudumia yatima hawa. Japokuwa ninajihusisha kwenye mambo mema, ninajikuta nimepoteza au kupuuzia muda wa kujifunza, ambalo si swala la hekima kwangu. Wiki iliyopita nilikumbushwa ya kwamba ninahitaji kuwekeza muda kuandaa kitu kutokea kwenye neno la Mungu kwaajili ya kuwalisha watu kila siku ya Jumapili.”

Yule mchungaji aliiweka kalamu yake chini kisha akamtazama Immanuel kwa macho yake yenye mng’ao na uhai. “Ninaitwa Petro.”

Immanuel alishangaa sana ya kwamba mchungaji Petro, pamoja na uzoefu wa zaidi

ya miaka ishirini na nne kwenye huduma ya uchungaji, bado alikuwa na shauku ya kujifunza! Immanuel alikusudia moyoni ya kwamba atadumu katika kujifunza wakati akiendelea na kulea kanisa.

Sauti ya mchungaji Petro ikasikika tena. "Ndugu yangu, unaweza ukanishirikisha kile ulichohubiri Jumapili iliyopita?"

Immanuel alijibu kwa haraka. "Nilitumia maandiko ambayo mwalimu wetu alitupitisha wiki iliyopita. Nilihubiri kutokea kwenye Matendo ya Mitume 14:23. Niliwaambia watu, 'Ndiyo, nitatumika kama mchungaji wenu mpya, lakini angalieni hapa Paulo alichagua wazee—wingi—ndani ya kanisa. Japokuwa nitatumika kama mchungaji wenu, tunahitaji viongozi wengi kanisani.'"

Immanuel alijisikia furaha na hali ya kuchangamka alipoendelea kumsimulia Petro. "Pia nilinukuu Matendo ya Mitume 20:28 na kufundisha ya kwamba ni lazima tuitambue kazi ya Roho Mtakatifu pindi anapoinua na kuchagua viongozi kwaajili ya kanisa."

"Safi sana," Petro alijibu kwa mshangao. "Unaonekana ni mtu mnyenyekevu. Ukiwafundisha watu wako vitu vinavyoeleweka

na vilivyowazi namna hii, Mungu atayatumia mafundisho yako. Kanisa lako litakuwa imara!"

Upendo wa Petro na shauku vilimgusa Immanuel na mara moja akatambua ya kwamba Mungu amempatia zawadi ya muhimu sana. Naweza kujifunza mambo mengi sana kutoka kwa Petro. Immanuel alimshukuru Mungu kimyakimya kwaajili ya rafiki yake mpya.

Darasa likiwa limejaa, mwalimu alisogea mbele ya darasa. Wanafunzi walipomuona walikaa kimya mara moja.

"Tuanze kipindi chetu," mwalimu alitoa maelekezo. "Leo, ninataka tuanze na vipaumbele vitatu vya muhimu kwa wale wanaochunga kanisa la Mungu."

Immanuel aliituliza miguu yake kwenye sakafu vizuri huku mkononi akiwa ameshikilia penseli yake, karatasi na Biblia tayari kwa kujifunza. Iwapo Petro bado anataka kujifunza pamoja na uzoefu wa miaka yote hiyo kwenye huduma ya uchungaji, Basi Immanuel hakuwa na njia nyingine isipokuwa kujifunza kwa umakini na kwakuwa ni mchungaji mchanga wa kanisa la Mungu.

## Sura ya Nne: Maswali

1. Immanuel alikutana na rafiki mpya kwenye darasa ambaye alikuwa na uzoefu wa miaka ishirini na nne kwenye huduma ya kuchunga kanisa la Mungu. Je, Immanuel aligundua Mungu amempatia nini kupitia huyu ndugu/Mchungaji Petro? Kwanini swala hili lilikuwa la muhimu?

2. Ni jambo gani umejifunza kutoka kwa wachungaji wenye uzoefu mwingi?

    a. Je, ni mambo gani ambayo Immanuel alijifunza wakati akizungumza na Petro?

b. Juu ya ulazima wa kuendelea kukua?

c. Juu ya kufundisha kanisa?

# Sura ya Tano:

## Hali ya Ibada Binafsi ya Mchungaji

### Ibada Binafsi kwa Mungu katika Maombi

Mwalimu alitembea kuelekea ubaoni na kuandika, Ibada Binafsi kwa Mungu katika Maombi. "Hii inawakilisha kipaumbele cha kwanza muhimu cha mchungaji," alitangaza, huku akiligeukia darasa. "Tunapaswa kuweka juhudi kuwa watu wa maombi wanaomtafuta Mungu. Biblia hii inatuonyesha mifano ya watu wengi waliotumika kama wachungaji kama vile Musa, Paulo, na Bwana Yesu. Kila mmoja wao aliwekeza muda wa ibada binafsi na Mungu kwa njia ya maombi. Kimsingi, nimeyahesabu zaidi ya maombi ishirini ya Musa! Si hivyo tu, Biblia inatuambia ya Mungu aliongea na Musa na kukutana naye zaidi ya mara mia moja na ishirini. Hii ni kutuonyesha ya kwamba maombi na mawasiliano na Mungu lilikuwa ni jambo la muhimu sana kwenye maisha ya Musa. Hebu mfikirie Musa namna alivyowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri. Biblia inaonyesha wazi ya kwamba aliyafanya haya kutokea kwenye mtiririko wa maisha yake ya maombi."

Immanuel alivuta pumzi ndefu. Je alifahamu umuhimu wa maisha ya maombi kwake binafsi? Ni kweli alimuona yule mchungaji wake mzee akiomba mara nyingi sana.

"Rafiki zangu wapendwa, fanyeni kama Musa alivyofanya," aliendelea mwalimu kufundisha. "Watu aliowaongoza walimuheshimu na kumfuata kwasababu aliwekeza muda wake binafsi kuwa na Mungu. Ndivyo itakavyokuwa kwetu. Lazima tuwekeze muda kwenye maombi binafsi. Kama una Agano la Kale, soma habari za Musa kwenye kitabu cha Kutoka. Utaona namna ambavyo Mungu aliyajibu maombi ya Musa kwa namna ya nguvu na ajabu sana mara nyingi. Hebu tutafute kitu cha namna iyo hiyo."

Mwalimua alichukua Biblia yake na kuifungua. "Mfikirieni pia Bwana Yesu. Tafakari ni mara nyingi kiasi gani alijitenga ili kupata wasaa binafsi na Mungu katika maombi. Hebu tusome maandiko kadhaa kwa pamoja." Immanuel aliifungua Biblia yake akaanza kuambatana na mwalimu alipokuwa akisoma.

> Naye Yesu aliposikia; hayo aliondoka huko katika chombo, akaenda Mahali pasipo watu, faraghani. Na mkutano waliposikia,

> walimfuata kwa miguu kutoka mjini mwao. (Mathayo 14:13)
>
> Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake. (Mathayo 14:23)
>
> Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani iitwayo Gethsemane, akawaambia wanafunzi wake, ketini hapa, hata niende kule nikaombe. (Mathayo 26:36)
>
> Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko. (Marko 1:35)

Moyo wa Immanuel ulikuwa ukidunda kwa kasi alipokuwa akiusikiliza ule mstari wa mwisho. Amekuwa akifanya jambo la namna hiyo pia! Amekuwa akienda kuchunga mifugo mapema sana, ili apate muda wa kukaa na Bwana.

"Hebu tazama Marko 6:31," mwalimu alielekeza. "Si tu Bwana alitumia muda wa maombi akiwa peke yake, alitumia muda wa kuwa na ushirika na wanafunzi wake kama vile Mungu alivyokuwa na ushirika na Musa.

Maandiko mengine ambayo unaweza kujisomea kwa wakati wako ni pamoja na Luka 5:16 na Luka 6:12."

"Kumbukeni hili," mwalimu aliendelea kufundisha. "Wanafunzi hawakuwahi kumuuliza Yesu namna ya kuhubiri, lakini walimuuliza Yesu namna ya kuomba! Walimuona Bwana akiomba, kitu ambacho kiliwavutia sana. Hebu tusikilize Luka 11:1 inavyosema:

> Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja wa wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufindishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake.'"

Mwalimu alipita katikati ya madawati huku akiwatazama wanafunzi wakati akitembea. "Hatujayagusa maandiko yote ambayo Bwana anafundisha juu ya maombi. Siku moja tutajielekeza kwenye mandiko hayo. Leo tunataka tukumbuke ya kwamba kulinda huduma tulizo nazo, tunapaswa kulinda maisha yetu ya maombi."

Mwanafunzi mmoja akanyoosha mkono wake. "Tunawezaje kuyafanya haya mwalimu?

Wengi wetu tunahitaji kufanya kazi za mikono na kutunza familia zetu pia."

"Ninashauri uwe unatembea na Biblia yako wakati wote na kutafuta eneo tulivu kwaajili ya kuomba mahali ambapo hauwezi kuingiliwa na kelele za watu. Inaweza kuwa ni nyuma ya nyumba yako, mahali penye mwamba. Muda unaouweka kwenye maombi unaweza kuwa ni mtaji mzuri sana kwaajili ya kujiandaa kufanya kazi zako za mikono na kuitunza familia yako."

Mwalimu alitembea kurudi kwenye ubao. "Nitaandika hapa muundo wa sehemu nne katika kuomba. Andikeni haya kwenye karatasi zenu na mziweke kwenye Biblia zenu ili muweze kukumbuka kila muendapo kwenye maombi."

Immanuel aliandika kwa umakini kila alichokisoma kwenye ubao:

1) Ni kwa namna gani ninaweza kuanza kwa kumsifu Mungu?
2) Mambo gani ninahitaji kutubia kutoka kwenye moyo wangu?
3) Mambo gani ya kumshukuru Mungu kwayo?
4) Ni kwa namna ani ninapaswa kumuomba mahitaji yangu kwa unyenyekevu?

Baada ya wanafunzi kumaliza kunakili, mwalimu alianza tena kufafanua. “Nyongeza juu ya hayo, tunahitaji kutengeneza orodha ya mahitaji ya kuombea na kuyaombea makanisa yetu mara kwa mara na mahitaji ya watu wetu. Mtu anapokuomba umuombee, andika hitaji hilo ili usisahau. Kisha omba. Hii inatusaidia kuwa waaminifu kwenye maombi yetu. Pia inatusaidia kujenga imani zetu.”

Huu muundo wa hatua nne za kuomba ulionekana ni jambo jipya kwa Immanuel. Ni kweli alikuwa anaomba mara kwa mara, lakini maombi yake yaliibuka tu pale alipoona tatizo au hitaji limejitokeza mbele yake. Sasa alitambua ya kwamba anapaswa kuyaelekeza maisha yake kwa Mungu haijalishi nini kilikuwa kinaendelea kwenye mazingira yake.

“Hebu acaha niseme jambo hili tena,” mwalimu alikazia. “Wale waongozao kanisa la Mungu imewalazimu kumtafuta Mungu katika maombi. Nimewahi kusikia mtu mmoja akisema kwamba maombi ndiyo njia mabayo Mungu ameivuvia ili kwayo tupate yote tunayoyahitaji kutoka kwenye mkono wa Mungu. Kumbuka mifano yetu kutokea kwenywe maandiko. Viongozi wakubwa na wachungaji tuliosoma habari zao walimtafuta Mungu katika maombi. Tunaweza

kuongeza kwenye hiyo orodha ya Musa, Samweli, Daudi, Eliya, Nehemia, na mitume wengi. Iwapo tutamtafuta Bwana katika maombi atatusaidia."

Immanuel aliweza kumsikia mwalimu kutokea ndani ya moyo ya kwamba somo hili analifundisha kwa kumaanisha. Mwalimu alivuta pumzi kisha akaendelea.

"Maandiko yanatuahidia hivi, 'Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa' (Luka 11:9). Tunapaswa kuomba tukiwa peke yetu, pia tunapaswa kuomba tukiwa na watu wetu. Tunapaswa pia kuomba kwa imani, tukitambua ya kwamba Mungu anasikia na kujibu maombi yetu. Tukifanya hayo, tutakuwa tunampa Mungu nafasi anayostahili kama kiini cha maisha yetu nasi tutapata njia kukielekea kiini cha mapenzi yake."

Immanuel aliyaruhusu mambo haya yazame ndani ya moyo wake. Alikuwa na uzoefu kwenye hili, alitambua. Aliomba ili kuelewa mapenzi ya Mungu juu yake kipindi kile amababapo wazee wawili walimfuata na kumuomba awe mchungaji wa kanisa la kijijini kwao. Na sasa yuko hapa alipo, ameketi kwenye darasa anajifunza maana ya kile alichokifanya. Mungu alipompatia rafiki mpya, Petro. Immanuel aliomba tena maombi mafupi ya shukurani kimyakimya.

## Ibada Binafsi kwa Mungu katika Neno

Mwalimu aliusogelea ubao kwa mara nyingine tena. Akafuta kila kitu alichokuwa amekiandika kuhusiana na maombi na kisha akaandika, "Ibada binafsi kwa neno la Mungu."

"Tusiishie kuomba tu lakini hebu tuwe na ibada binafsi kwenye neno. Mamlaka ya kuongoza kanisa la mahala pamoja inatoka kwa Mungu, lakini mamlaka hiyo hubaki kuwa halali na inayotambulika iwapo tutadumu na kutenda kwa mujibu wa neno la Mungu. Kama wachungaji wa kanisa la Mungu, *sisi siyo:*

- viongozi wa kimila;
- wanasiasa;
- wafalme.

Kama wachungaji wa kanisa la Mungu, *sisi ni:*

- tunaishi chini ya serikali ya Mungu;
- tunafuata Neno la Mungu wakati wote;
- tunajifunza, tunapokea maarifa na tunafuata neno katika kila tufanyalo."

"Neno la Mungu ndiyo mamlaka kuu. Hakuna mwanadamu ambaye anaweza kuchukua hiyo mamlaka. Hebu sikilizeni Zaburi 119:89. 'Ee BWANA, neno lako lasimama Imara mbinguni hata milele' Katika Agano Jipya Yesu alisema,

‘Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.’ (Luka 21:33). Kwahiyo, huduma zetu lazima zijikite kwenye neno la Mungu.”

Immanuel alitamani angekuwa amebeba penseli mbili za kuandikia leo. Kwasababu kwa mwenendo wa darasa inawezekana penseli aliyobeba ikabaki kama ncha ya mbao. Karatasi na kichwa chake vilikuwa vimejazwa tayari, lakini mwalimu alionekana bado ana mengi ya kufundisha!

“Tunaweza kuweka haya katika utekelezaji kwa namna mbili. Kwanza, tunahitaji kulisha roho zetu kwa neno la Mungu. Warumi 10:17 inatuambia ‘imani huja kwa kusikia na kusikia neno la Kristo.’ Kusoma na kutafakari neno la Mungu kila siku huifanya imani yetu ikue na hutufundisha namna ya kuishi. Kufanya hivi pia kuepukana na hali ya kukata tamaa au kuondoka kwenye njia sahihi. Inatuepusha na maisha ya ubaridi wa kiroho. Wakolosai 3:16 inasema ‘neno la Kristo na lijae kwa wingi ndani yenu…’”

Mwalimu alipumzika kidogo ili kutoa nafasi ya kila mwanafunzi kusikiliza maneno yake yaliyokuwa yanafuatia. “Iwapo neno la Mungu halimo ndani yetu kwa wingi, tuna nini cha

kuwafundisha watu wengine? Kila mmoja wenu awe na ibada binafsi kwa neno la Mungu!"

"Pili, tunaona ya kwamba mahubiri na mafundisho yetu yote yanatokana na neno la Mungu, si katika mitazamo na maoni yetu. Hatupaswi pia kusimulia hadithi tu."

"Wachungaji pia huwatembelea wagonjwa na kutoa huduma ya ushauri kwa watu wenye mahitaji mbalimbali. Watu hawa wanahitaji tuwasomee Maandiko na kuwaelekeza namna ya kumtumainia Mungu. Wachungaji hufundisha juu ya wokovu na dhambi. Huduma yote hii lazima ijikite kwenye neno la Mungu."

Mwalimu alijiegamiza kwenye dawati moja ambalolilikuwa halijakaliwa na mtu na akawa katika mwonekano wa kimsisitizo. "Wachungaji wa kanisa la Mungu, hufundisha neno lake la thamani. Kumbukeni kile amabacho mtume Paulo alimwambia yule kiongozi wa kanisa mwenye umri mdogo, Timotheo. 'Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema' (2 Timotheo 3:16-17). Na baadaye tunasoma, 'Ninakuagiza mbele za Mungu, na mbele za

Kristo Yesu… lihubiri neno, uwe tayari, wakati unaofaa na wakati usiofaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na Mafundisho' (2 Timotheo 4:1-2)."

"Kwa hiyo, hatusomi neno la Mungu kwaajili ya kuzijenga imani zetu binafsi, tunahitaji kuwashirikisha wengine kwa uendelevu ili kuzijenga imani zao pia. Hiki ndicho kinachomaanishwa na na Biblia isemapo juu ya 'wajitaabishao kwa kuhutubu na mafundisho' (1 Timotheo 5:17). Sina namna bora zaidi ya kulifafanua hili zaidi ya hii: Kama viongozi wa kanisa tunapaswa kuyajenga maisha yetu binafsi na huduma zetu katika msingi wa neno la Mungu."

Immanuel alijisikia hali ya ahueni mwalimu alipotangaza ya kuwa ni kipindi cha mapumziko na kupata chai. Alidhani ya kwamba mambo yamekuwa mengi kiasi kwamba hayatoshi tena kwenye kichwa chake. Petro na Immanuel waliamua kunywa chai pamoja.

"Si nilikuambia ya kwamba huyu mwalimu ni mzuri sana?" Petro alimchokoza Immanuel. "Ninaamini kuna mawazo yatokanayo na darasa la leo yanaweza kukufaa kuandaa mahubiri yako."

Immanuel alitikisa kichwa huku akiegamia ukuta. Alikuwa amejawa na mambo mengi sana

ya kutafakari kwaajili yake yeye mwenyewe binafsi lakini pia mambo ya kuwashirikisha watu wa kanisa lake.

### Kutoa Mwongozo wa Kiroho kwa Wengine

Immanuel na Petro walirejea kwenye nafasi zao za kuketi baada ya mapumziko mafupi ya chai, tayari kusikia mafundisho mengi zaidi.

Mwalimu alisimama na kuchukua nafasi yake mbele ya darasa. "Ninajua akili zenu zinaweza kuwa kama zimejaa baada ya masomo yote asubuhi ya leo, lakini hatuwezi kujazwa na kukosa nafasi ya kuweka neno la Mungu."

Immanuel alisikia minong'ono kadhaa Kutokea kwa watu waliomzunguka.

"Tumezungumza juu ya maeneo mawili ya kuyaelekea ambayo mchungaji anapaswa kuwa nayo—maisha ya ibada binafsi katika maombi na ibada binafsi katika neno la Mungu. Sasa ninawaletea jambo la tatu kwaajili ya kazi ya kichungaji. Kiongozi wa kanisa la mahala pamoja anapokea fursa nyingi sana za kufundisha na kuwapa miongozo ya kiroho watu wengine."

"Hebu fikiria matukio mengi ambayo watu humualika kiongozi wa kanisa," mwalimu alitoa changamoto. "Huwahubiria waamini kila Jumapili na kuna nyakati ambazo huwahubiria

watu mitaani au kijijini. Siku moja baadaye anaenda kumtembelea mgonjwa au mtu mwenye mahitaji. Labda anaongoza kipindi cha kusoma neno au maombi pamoja na washirika wa kanisa lake. Inawezekana akapewa kuongoza ibada ya maziko au msiba, na wiki hiyo hiyo akafungisha ndoa ya vijana. Atabatiza waamini wapya na kuwabariki watoto wadogo waliozaliwa. Nyongeza ya hapo, anaweza kuwa anasaidia miradi ya kijamii, na kutoa mwongozo kwenye matukio muhimu."

"Ooh," Immanuel alipigwa na butwaa. "Ndiyo, kutumika kama mchungaji ni jukumu lilobeba mambo mengi ndani yake!"

"Kuna somo hapa," mwalimu alianza kutoa maelezo. "Matukio yote hayo yapo kama fursa kwa mchungaji kutoka mwongozo wa kiroho au kuwaonyesha watu namna ya kutambua mapenzi ya Mungu. Maarifa yetu juu ya neno la Mungu yanapaswa kutiririka na kuwa manufaa kwenye matukio haya muhimu."

Mwalimu alipokuwa akitembea tena, kwenda na kurudi katikati ya madawati, Immanuel alihisi ya kwamba kila mmoja amebeba masomo na kuyajaza kwenye moyo wake kwa tafakari kubwa.

"Haijalishi watu wanakuja kwetu wakiwa kwenye hali ya maumivu na mambo magumu

au nyakati za furaha na shangwe, tunapaswa kuwapatia neno la Mungu. Katika uongozi wetu wote tunapaswa kudhihirisha wazi ya kwamba tunalielewa neno la Mungu na tunalichukulia kwa uzito wa hali ya juu. Mungu alitupatia jukumu hili, ili kuwaelekeza watu wake kwenye neno lake, kusababisha watu wamwamini Kristo, na kuwaongoza watu katika wokovu na maisha ya kumuishia Kristo kikamilifu. Matukio yote haya yana jambo moja linalofanana—kupitia hayo tunawafundisha watu wote namna ya kuishi kama watumishi wa Mungu."

"Kuwafundisha wengine huwa hakutokei kila mara kwa mtindo ule wa moja kwa moja, kutoa amri kama tunavyokuwa tukihubiri. Inaweza kutokea pia katika hali ya upole na utulivu na roho ya kuchukuliana. Mchungaji mwema huwaendea watu ili kuwaonyesha upendo, lakini kuwapelekea neno la Mungu. Husikiliza watu na kuzungumza nao, huwashirikisha neno katika namna ambayo itawasaidia na kuwafaa. Biblia huuita muundo huu Ufuasaji. Bwana wetu anatuelekeza tutimilize jukumu hili kwenye Mathayo 28:19 anaposema, 'na kuwafanya kuwa wanafunzi…'"

Kabla kipindi hiki cha pili hakijafika tamati, mwalimu aliwapa nafasi wanafunzi, kila mmoja

alishirikishe darasa nyakati ambazo alihitajika kutoa mwongozo wa kiroho. Immanuel alitoa ushuhuda wake wa namna alivyotoa neno kwa ufupi wakati wa msiba wa mchungaji wake. “Nilitaka kuleta tumaini na tulizo kwa watu waliompoteza mwalimu wao mpendwa wa muda mrefu,” alisema.

Petro naye alitoa ushuhuda wake. Alielezea wakati ambapo raisi wa nchi yao alimwalika aongoze maombi kwenye sherehe fulani maalum. Petro alisema, “Nilijikumbusha kila mara ya kwamba kama nilivyo mimi, ndivyo ambavyo raisi naye ni mwanadamu na anamuhitaji Mungu kama walivyo wanadamu wengine. Nilimuombea kwamba apate neema ya kumjua Mungu na kuyajua mapenzi yake.”

Mwananfunzi mwingine alisema ushuhuda wake ambapo siku moja alisimama pembezoni mwa kaburi la mtoto mchanga, na alisoma neno la Mungu, na kuwaombea watu wenye huzuni ya kupoteza mtoto wao mdogo, mzaliwa wao wa kwanza.

Immanuel alijaribu kuiwaza ile huzuni wapatayo watu wanapokuwa makaburini. Ni jambo gumu kusimama na wazazi wa marehemu kwenye wakati huu wa maumivu. Immanuel aliendelea kutambua ya kwamba

huduma ya mchungaji huleta matukio mengi ambayo inaweza kuonekana ya kwamba kutoa mwongozo wa kiroho ni jambo gumu.

Mwalimu alikuwa kama vile ameyasoma mawazo ya Immanuel. "Huduma inaweza kutuleta kwenye nyakati ngumu," alisema. "Lakini Mungu hutupa nguvu na hutupatia neno lake. Hatujitoi sisi wenyewe kwa watu bali pamoja na sisi tunawapa Mungu wetu na neno lake. Msisahau hilo!"

Mawazo mengi yaliendelea kutembea kichwani mwa Immanuel alipokuwa akiendesha baiskeli kurudi kijijini kwao siku hiyo ya Jumatatu. Hali ya mazingira ya kijijini ilipita bila kuitambua kwasababu alikuwa amezama kimawazo. Kuna gari lilimkaribia sana wakati akiwa njiani, nalo hakuliona.

Ninahitaji kupangilia zaidi mara kwa mara namna ya kutenda kama mchungaji, alikusudia moyoni mwake. Immanuel akatengeneza orodha ya maswala muhimu kichwani mwake, kama vile mwalimu wao alivyokuwa akifanya pale ubaoni.

1) Ninahitaji kuwa na muda binafsi na Mungu kwa njia ya maombi.
2) Ninahitaji kuwekeza muda kwenye neno la Mungu.

3) Ninahitaji kujiandaa kwa fursa ambazo Mungu anazileta mbele yangu kufundisha.

Nitayatimiliza vipi yote hayo, Immanuel alijiuliza mwenyewe! Aliipitia tena orodha ya majukumu yake, hii ni pamoja na kazi zake za nyumbani na kuchunga mifugo ya baba yake. Hakuna hata moja lilipaswa kubadilika. Aligundua ya kwamba kwenye majukumu yote ya maisha yake alipaswa kuomba, kusoma neno la Mungu na kujiandaa. Alipaswa kuwa makini juu ya kazi yake, lakini alipaswa kuwa makini pia na kazi ya Mungu.

Alipokuwa akiendelea kuendesha baiskeli yake, akafika kwenye barabara iendayo kijijini kwao. Kuna orodha mpya ilikuja mawazoni mwake.

1) Ninaweza kuchagua jioni kadhaa na kuzitumia kuandaa masomo ya Jumapili.
2) Ninaweza kuwatembelea wagonjwa na wahitaji baada tu ya kuwafunga mifugo kwenye zizi lao.
3) Ninaweza kuongea na baba yangu kumuomba aniongezee siku moja ya mapumziko tofauti na siku ya Jumapili ili nitumie muda kufanya shughuli za kanisa. Labda ninaweza kufanya hivyo siku za Jumamosi.

Immanuel alishikwa na furaha kubwa. Kama anavyoweza kupangilia, na Jumamosi akipata ruhusa ya kuitumia kwaajili ya huduma, anaweza kukutana na washirika wa kanisa siku hizo. Anaweza kuandaa matukio na kutumia muda unaobaki kujiandaa kwaajili ya ibada za Jumapili.

Immanuel alitambua ya kwamba alikuwa anafanya kazi nzuri sana eneo la maombi na kusoma neno la Mungu. Kwa siku nyingi, baada ya kutoa mifugo na kuifikisha machungani, aliwekeza muda wake kwenye mambo haya mawili.

Immanuel alipokuwa akikaribia nyumbani kwao alijisikia jambo moja lilokuwa linawaka moyoni mwake. Alikuwa na shauku kubwa ya kuwafikia wengine kwa habari njema za Yesu, hususani vijana. Labda angepaswa kuandaa kikundi kidogo ili kianze huduma ya kuwafikia watu kijijini.

Immanuel aliiegesha baiskeli yake ukutani. Safari ya kurudi nyumbani ilizalisha mpango ndani ya moyo wake ili kumuwezesha kuchunga na kustawisha kanisa la Mungu. Siku hii ya darasa ilijaza daftari lake na kichwa chake, na kumsaidia kukua zaidi katika wito wake mpya kama mchungaji wa kanisa la Mungu.

# Sura ya Tano: Maswali

1. Orodhesha vipaumbele muhimu vitatu vya mchungaji wa kanisa la Mungu:

   1. ____________________
   2. ____________________
   3. ____________________

2. Kati ya mambo haya mitatu, ni jambo gani amabalo linakuwia gumu kuliishi katika utumishi wako?

   ❑ □Ibada binafsi kwa Mungu katika maombi.
   ❑ Ibada binafsi kwa Mungu katika kusoma neno.
   ❑ Kutoa mwongozo wa kiroho.

3. Immanuel aliyatafakari majukumu na kisha akaanza kupangilia namna ya kutekeleza vipaumbele vyote vitatu katika wiki yake. Tumia nafasi uliyopewa chini kufanya vivyo hivyo.

   Kazi na shughuli zingine zinazoweza kunichukulia muda wangu sasa:

   ____________________

   ____________________

Kipindi gani ninaweza kuuweka muda wangu wa kuomba kwa bidii?

Ni wakati gani ninaweza kupangilia swala la kusoma neno la Mungu kwa shauku?

Ni kwa namna gani ninaweza kuupangilia muda wangu ili kutoa mwongozo wa kiroho kwa wengine?

Ni shughuli/matukio gani ninapaswa kuyaandaa kama majukwaa ya kutoa mwongozo wa kiroho kwa wengine (mfano mikutano, au kuwatembelea wagonjwa)?

# Sura ya Sita:

## Tabia ya Mchungaji

Immanuel alimsalimia Petro wakati anaketi chini ili kuanza darasa la tatu kwenye mfululizo wa mafunzo yao. "Umekuja tena," alisema Immanuel.

"Ndiyo hivyo," Petro alimjibu. "Na nimewaleta wale wachungaji vijana pamoja name." Petro aliwatambulisha wale wachungaji kwa Immanuel, naye akawasalimu kwa upole kwa kuwapa mkono. Alitiwa moyo baada ya kuwaona ni watu ambao bado hawajapata uhakika kama aliokuwa nao yeye!

Kama vile alikuwa anamsoma mawazo yake, Petro alisema. "Ni vyema kubaki katika hali ya unyenyekevu wakati tunajifunza na kukua pamoja. Hakuna mtu ambaye hufika mwisho katika maisha ya ukristo mpaka tufike mbinguni. Pungufu ya hapo, tunaendelea kukua kila siku, ndiyo hivyo."

"Amina," waliitikia wachungaji wale watatu kwa pamoja.

"Njooni mkae," Petro aliwakaribisha rafiki zake. "Tujiandae kuona kile ambacho mwalimu wetu ametuandalia leo." Immanuel alijisikia hali

ya matarajio kama alivyozoea wakati anatoa Biblia, daftari, na penseli mbili kama tahadhari.

Mwalimu alianza kwa swali la udadisi. "Kiongozi wa kanisa anapaswa kuwa mtu wa namna gani – mkristo wa namna gani? Tumezungumza kwa kina juu ya yale ambayo mchungaji wanapaswa kuyafanya. Lakini mchungaji anapaswa kuwaje? Tunajua anaishi kama kielelezo kwa kundi lake. Tunajua Paulo anafundisha kimaalum juu ya hili kwa mchungaji kijana Timotheo, 1 Timotheo 5. Lakini ni mtu wa namna gani anapaswa kuwa na tabia hiyo?" Macho ya mwalimu yalionyesha kuachilia changamoto na Immanuel alikuwa makini sana kusikiliza.

"Ashukuriwe Mungu," mwalimu aliendelea, "Neno la Mungu linatupa orodha mbili ndefu kwenye 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:6-9 ambazo zinajibu maswali yote haya. Ninataka niwashirikishe baadhi ya mambo. Hebu tuanze."

Immanuel alinakili kwa haraka maandiko yote ambayo mwalimu aliyataja, ili aweze kuyasoma kwa umakini atakapokuwa nyumbani akijisomea.

## Shauku Njema

"Hebu tusome 1 Timotheo 3:1." Sauti ya mwalimu ambayo ilikuwa imezoeleka tayari

ilikijaza kile chumba cha darasa wakati akisoma maandiko. "Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema."

"Kuwa mchungaji wa kanisa la Mungu inahitaji kuwa na wito kutoka kwa Mungu mwenyewe. Mungu huachilia mwito wa ndani ya moyo wa mtu husika ya kwamba maisha yake yanapaswa kuelekea uelekeo huu. Tumetoka kusoma ya kwamba shauku ya kutenda kazi kama mwangalizi inawakilisha shauku njema, ya nguvu na ya muda mrefu. Shauku hii hutupitisha katika siku ngumu. Tunapigana vita njema ya imani kwasababu tunajua ya wa kwamba Mungu anatutaka tufanye hivyo. Andiko hili hutufanya kila mmoja wetu kujiuliza maswali: Je, Mungu ndiye aliyenipa hii shauku takatifu? Je, shauku yangu imekuwa endelevu au baada ya muda fulani imepotea? Je, kuna watu wengine ambao wananithibitishia ya kwamba Mungu ameniita kufanya kazi ya uchungaji?"

Immanuel alianza kuifikiria safari yake mwenyewe. Ndiyo, akajiwazia. Nina shauku na utumishi huu, Mungu nisaidie. Ninataka kumpendeza Mungu, kuvuna roho, na kulijenga kanisa la Mungu. Immanuel aliikumbuka ile siku ambayo wazee wawili walimfuata na kumuomba ajaze ile nafasi ambayo mchungaji

ameiacha. Aliona ni kwa namna gani Mungu amekuwa akiiikuza shauku yake na kumtia nguvu katika kufundisha tangu siku hiyo.

Mwalimua aliwatazama wanafunzi wake. “Kile ninachokizungumzia kutoka kwenye neno la Mungu kinaelezea matamanio mazuri, ya kumpendeza Mungu na kutunza kundi lake. Matamanio haya hutufanya tuwe na juhudi, tujiandae, na kukua, na matamanio haya huwa ni endelevu siku zote za maisha. Je, kila mmoja wenu ana hiyo shauku takatifu?”

Immanuel aliyaandika maneno yale, “Ndiyo, nina shauku ya kulitumikia kanisa la Mungu na kutunza kundi lake,” pembeni ya daftrai lake, kisha akaongezea na tarehe. Alitaka atunze huu wasaa kipindi atakapokuwa akitekeleza safari ya maisha yake yote ya uchungaji.

## Vigezo vya Ujumla

“Sasa, kwa kuwa tunajua ya kwamba kuna shauku ya kudumu inapaswa kuwepo kwaajili ya uchungaji, Biblia inaeleza ni viezo gani ambavyo mchungaji mzuri anapaswa kuwa navyo na kuviendeleza? Kuna vigezo vya wali tunaweza kuviita vigezo vya ujumla. Hebu tusome maandiko ili tuweze kujifunza juu ya hayo. Fungua 1 Timotheo 3:6. Orodha ya

vigezo hivi hapa kimsingi inaanzia mstari wa pili, lakini tutarukia katikati, moja kwa moja kwenye mstari wa sita."

Immanuel alifungua alisikia kurasa za Biblia zikifunguka na yeye alifungua Biblia yake.

"''Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi," mwalimu aliwasomea. "Hii ni sawa na kulinganisha na Tito 1:7, ambayo inasema mwangalizi anapaswa kuwa 'mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu.' Kwahiyo muda wa kukomaa ni muhimu ili mtu akue na kutambua uzito na ukubwa wa kazi ya kuchunga kanisa la Mungu. Mtu hapaswi kuirukia kazi hii bila maandalizi."

Immanuel alipumzika kidogo ili kuelewa yaliyosemwa, moyo wake haukuwa na uhakika, mimi ni kijana mdogo, alijiwazia. Je, kweli niko tayari kwaajili ya kazi hii? Immanuel alijifuta kwenye paji lake la uso. Je mimi kweli nina vigezo ambavyo mwalimu amevizungumza? Hii ni hatua muhimu, alijisemesha mwenyewe. Nina shauku ya kuifanya kazi hii, lakini ninahitaji kupata uthibitisho kutoka kwa watu wengine. Japokuwa watu kutoka kanisani kwao walimtafuta na kumuomba awe mchungaji, lakini Immanuel aliweka nia ya kwenda kuzungumza nao tena.

Mwalimu aliendelea. “Mchungaji anapaswa kudhihirisha uwezo wa kufundisha (1 Timotheo 3:2) huku ‘akilishika lile neno la imani’ (Tito 1:9). Tumezungumza kwa kirefu sana ni kwa namna gani neno ni kitovu cha huduma ya kiongozi wa kanisa. Ndiyo, kiongozi wa kanisa anapaswa kudhihirisha kipawa na uwezo wa kushirikisha watu wengine neno kwa uwazi. Hili linaweza kuonekana kwenye mazingira mbalimbali, kupitia mahubiri ya Jumapili mpaka kumsomea na kumshauri mtu mwenye changamoto.”

Mwalimu aliliangalia darasa. “Mambo mengi zaidi yanaonekana kwaajili yetu kwenye I Timotheo sura ya tatu na Tito sura ya kwanza. Nitaorodhesha zaidi vigezo vya ujumla hapa ubaoni na kuweka maandiko ya rejea, ambayo yatawasaidia kujisomea hapo baadaye.”

- Mchungaji anapaswa kuwa ni mtu anayeiongoza nyumba yake katika utaratibu mzuri (1 Timotheo 3:4-5; Tito 1:6).
- Ndoa ya mchungaji inapaswa kung’ara kama mfano kwa wengine (1 Timotheo 3:2; Tito 1:6).

“Ninataka niwekeze muda kuzungumzia swala la ndoa na familia. Si vyema kabisa kwa kiongozi wa kanisa la Mungu kuwa mfano mbaya wa

kifamilia kwa wengine. Mtu anaweza kujisikia ya kwamba ameitwa, lakini iawapo hana ndoa ya Kikristo iliyo njema, iwapo upo kwenye ndoa, huwezi kupata heshima kutoka kwa watu wengine. Kila kiongozi wa kanisa unapaswa kuwafundisha na kuwaelekeza wote walio nyumbani mwako, wakionyesha uaminifu na unyoofu. Maandiko yanasemaje? Hebu tusome 1 Timotheo 3:5: 'yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?' Kumbukeni hili mnapoendelea kuishi na wenzi na watoto wenu. Hata maisha yako ya kifamilia yanawafundisha wengine kuhusu Mungu na yanafunua iwapo unaishi maisha ya uaminifu na ya unyoofu."

"Wachungaji huonyesha ushuhuda mwema kwa wale walio kwenye jamii ambao si washirika wa kanisa," mwalimu aliendelea kufundisha. "Tazama 1 Timotheo 3:7. 'Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.' Mchungaji anaishi katika jamii yake kama mtu mwema, mtu ambaye anaishi kwa ukweli na uadilifu katika mambo yote ayafanyayo."

Immanuel akakumbuka tukio moja wakati wa utoto wake. Siku moja alishuhudia ajali kule kijijini kwao. Alisimama akimtazama binti

mdogo, aliyekuwa amegongwa na gari kubwa lilokuwa likipita, alikuwa amelala kando ya njia huku akiwa ameumizwa. Umati ukakusanyika. Watu wengi alimzonga dereva na kumtishia uhai wake. Yule mchungaji mzee, ambaye kwa wakati huo Immanuel hakuwa anamjua sana, aliingilia kati na kusihi kuwe na hali ya utulivu. Alizungumza na binti aliyejeruhiwa na kuwashauri wote waliokuwepo kwenye lile tukio wampeleke kwanza yule binti kwenye zahanati. Kisha akasimama na kunyoosha mkono wake kuashiria kuwe na utulivu kwenye lile kusanyiko lililokuwa limejaa hasira, aliongea nao kwa utulivu na kwa umakini.

Immanuel alitambua sasa ya kwamba yule mchungaji wake mzee alikuwa ni mtu mwenye kuheshimiwa pale kijijini kwao. Waananchi wenye hasira walimsikiliza kwasababu aliishi maisha yenye kuvuta heshima ndani ya jamii. Immanuel alikusudia kuishi maisha yatakayovuta heshima kutoka kwa watu ndani na nje ya kanisa.

Mwalimu aliliachia darasa changamoto kabla hajawaruhusu kwenda kwenye mapumziko ya chai. "Tunaona kutokea kwenye maandiko haya ya kwamba kiongozi ameitwa kuishi maisha ambayo watu wengine wanapaswa kuyaiga.

Maisha haya ya mfano wa namna hii yanapaswa kuonekana katika nyumba yako, kanisani na kwenye jamii."

Mwalimu aliiweka Biblia yake kwenye dawati. "Pateni muda wa kupumzika na kunywa chai na kisha tukirudi tutaendela kujifunza vigezo vingine mahususi juu ya mchungaji."

Kwa mara nyingine tena Immanuel aliungana na Petro, safari hii na wale wachungaji vijana aliotambulishwa kwao awali nao walikuwepo. Alifurahi nafasi ya kushirikishana mawazo juu ya kile ambacho kila mmoja amejifunza.

## Mahusiano

Mwalimu hakutaka kupoteza hata sekunde moja, pindi wanafunzi wote waliporudi na kuketi kwenye nafasi zao. Tena, alifungua kwenye 1 Timotheo 3 na Tito 1. Immanuel ilibidi aweke alama ya karatasi kwenye haya maandiko kwenye Biblia yake. Alijua fika ya kwamba atahitaji kuyapitia maandiko haya mara nyingi kwa kadiri inavyowezekana.

"Sasa tutajielekeza kuzungumza namna mabvyo mchungaji hujenga mahusiano," mwalimu alisema. "Nitawapatia orodha fupi na maandiko ya rejea kwa kila kipengele."

Kwa mara nyingine tena penseli ya Immanuel

iliisha kwa vile alivyokuwa ananakili maandiko na kila mafundisho yaliyoandikwa ubaoni na mwalimu.

Mwangalizi ni mtu mkarimu (1 Timotheo 3:2).

Mwangalizi ni mtu mpole asiyekuwa na vurugu au magomvi (1 Timotheo 3:3; Tito 1:7).

Mwalimu alijielekeza kwenye kipengele cha pili. "Biblia inasema ya kwamba viongozi wa kanisa hawapaswi kuwashambulia watu wengine au hata kujihusisha na mabishano yasiyo na maana. Mambo magumu yanapoibuka, waangalizi wajifunze kutatua migogoro bila kubishana hata kama wanaona wamechokozwa."

Immanuel aliendelea kuguswa. Akakumbuka nyakati ambazo alipandwa na hasira na kujibizana na watu wengine, bila kujali ya kwamba matendo yake yanaendana na neno la Mungu. Alitambua wazi ya kwamba kwenye eneo hili anahitaji marekebisho.

"Hupaswi kukichukulia kwa wepesi kile kipengele cha kwanza," mwalimu aliendelea. "Waangalizi hufungua milango kwa watu ndivyo inavyopaswa kuwa kwetu, ili tuwe na mahusiano mazuri na watu wengi iwezekanavyo. Hata hivyo, huo ndiyo mwelekeo wa kusudi la kanisa kuwafikia watu wengi na kuwajenga katika imani."

"Fikiri juu ya hili. Tofauti na Mungu, ni mambo mawili tu yanadumu milele: Neno lake na watu. Kwahiyo ni hekima, kufuata na kufundisha maandiko hali tukijenga mahusiano na watu. Kwa kufanya hivyo, tunajielekeza kwenye mambo ya kudumu ambayo Mungu ameyaweka duniani."

## Ukomavu

"Ninajua mnaweza kuwa mmeshachoshwa na maswala ya orodha kwa sasa," mwalimu aliwatia moyo. Wanafunzi kadhaa darasani walicheka. "Biblia inatufundisha zaidi kuhusu maisha ya kiungu ya mwanagalizi. Ni muhimu tukatazama haya pamoja na kwamba tayari tuna orodha ndefu!"

Mwalimu alipiga hatua kurudi nyuma ulipo ubao. Chaki ikaanza kutembea kwenye ubao wakati penseli ya Immanuel ikitembea kwenye daftari lake.

- Viongozi wa kanisa huwa si watu wa kileo, wenye kiasi na mwenendo mwema (1 Timotheo 3:2; Tito 1:8).
- Viongozi wa kanisa hujizuia kuwa watu wa kuzoelea kileo (1 Timotheo 3:3; Tito 1:7).
- Viongozi wa kanisa hujitenga mbali na swala la kupenda fedha ambazo

huathiri hali yao ya kumpenda Mungu (1 Timotheo 3:3; Tito 1:7).

Mwalimua aliweka chini chaki na kuligeukia darasa. "Hebu tuzungumze kwa kina kiasi kuhusiana na vipengele hivi. Hebu tazameni kipengele cha kwanza. Tunawezaje kubaki kwenye mwito wetu iwapo tutakuwa watu wa kuharakisha au tabia zisizo na kiasi? Je, huoni tunapaswa kubaki chini ya uongozi wa Mungu muda wote? Kama ambavyo mnaweza kuwa mmeshuhudia, mchungaji mzuri huwa anaweza kuhitajika kutoka huduma kwa wengine muda wowote mchana au usiku. Watu wanaokuzunguka wanahitaji kujua iwapo wanatakiwa kukuamini, kwamba uko chini ya uongozi wa Mungu muda wote na uko tayari kuwasaidia. Hata hivyo, maisha yako ni mali ya Mungu na ya kundi ulilopewa kulitunza. Achana na mambo ambayo yanatilia mashaka au yanaibua maswali na tabia za namna hiyo, kwa utukufu wa Mungu. Maisha ya mchungaji yanapaswa kuwa wazi na matakatifu."

Immanuel alijiwazia ya kwamba hii kazi inahitaji kujitoa dhabihu kwa kiwango cha juu. Kisha akawaza jinsi ambavyo Bwana wake Yesu Kristo alivyotoa yote alijidhabihu kwaajili yake,

mwenye dhambi. Kweli, angeweza kuishi maisha ambayo yanampendeza Mungu, mwenye utayari kulihudumia kundi, kwa utukufu wa Yesu!

"Vipengele viwili vya mwisho kwenye hii orodha vinahusika na maswala ya mvinyo na fedha. Watu wengi huruhusu mambo haya yawarubuni. Kama wachungaji na waangalizi, hatupaswi kuruhusu hilo. Haya maeneo ambayo yamewakwaza na kuwangusha wengi hayapaswi kutuzuia ili tusionyeshe maisha ya kielelezo cha kiungu."

Mwalimu alipita katikati ya madawati wakati akiendelea kufundisha, kitu ambacho Immanuel alikuwa anakifurahi kwasababu alikuwa anajisikia hali fulani ya ukaribu na mwalimu wake katika kujifunza. "Sisi sote, kama viongozi wa kanisa, hatupaswi kujihusisha na mvinyo. Tunapaswa kujitenga na kilevi cha aina yoyote, iwe ni pombe au madawa. Pia, kama viongozi wa kanisa hatupaswi kuiruhusu mioyo yetu iwe na uroho wa pesa. Wito huu hauhusiani na watu wanaotaka kujipatia utajiri. Kama lengo lako ni kujipatia utajiri, nenda ufanye kitu kingine."

Mwalimu aliwakazia macho mwanafunzi mmoja mmoja. "Mchungaji mkomavu huzitazama pesa kama zilivyo—karatasi tu.

Kiongozi mkomavu hujitafutia ridhiko katika maisha ya kawaida ya kupata chakula, mavazi na mahali pa kujisitiri kama Yesu alivyofundisha. Tujifunze kumshukuru Mungu kwa kile alichotupatia badala ya kuwa waroho."

Mwalimu alipumzika ili aweze kuweka msisitizo juu ya kile anachotaka kukisema. "Vyote, fedha na kileo vinaweza kuwageuza watu walio huru kuwa watumwa. Hebu tubaki kuwa watumwa wa Bwana mmoja, Yesu Kristo."

"Lakini mwalimu," mwanafunzi mmoja aliinua sauti yake. "Mchungaji anapaswa kuishi maisha yaliyokamilika muda wote bila makosa? Ni nani anaweza kufanya hivyo?"

Mwalimu alitabasamu. "Ninafurahi ya kwamba umeuliza swali hilo; ni swali zuri! Hapana, hatuwezi kuishi maisha makamilifu, lakini tunaweza kutarajia kuishi maisha yasiyo na lawama. Hilo ndilo neno ambalo Biblia inalitumia hapa kwenye 1 Timotheo 3:2 na Tito 1:6. Hebu nikupatie mfano juu ya kile kinachomaanishwa hapa. Kwenye Agano la Kale, makuhani waliwasilisha mwanakondoo asiye na mawaa kwaajili ya dhabihu mbele za Bwana. Hakuna kondoo ambaye ni mkamilifu, lakini kuhani alitafuta kondoo ambaye hakuwa na ulemavu au mapungufu yanayoonekana."

Immanuel alielewa kwa mfano huo. Amekuwa mchungaji wa mifugo ya baba yake kwa muda mrefu kutambua ya kwamba kuna mifugo huonekana wamejeruhiwa ama kwa kushambuliwa na wanyama wengine au hata kugongwa na baiskeli. Kuna ambao walikuwa vizuri bila makovu ya namna hiyo. Lakini hii inahusianje na viongozi?

"Viongozi hawataishi maisha makamilifu," alielezea mwalimu. "Lakini tabia zao zinaakisi vigezo tulivyojifunza leo. Maisha yao yanaonyesha mfumo wa maisha yenye unyoofu yasiyolaumika. Hiyo ina maana ya kwamba hakuna mtu anayeweza kumtazama kiongozi na kumnyooshea kidole kuwa ana kovu linaloonekana. Hebu achana na alama ya kovu inayotokana na maisha mabaya na machaguo mabaya. Ndiyo, hii ni changamoto kubwa. Ukiiweza changamoto hii kubwa, utapokea baraka kubwa vilevile."

Darasa lilifikia ukomo kwenye kipengele muhimu kilichovuta umakini wakati wanafunzi wakiendelea kuitafakari vyema changamoto iliyo mbele yao ya kumuwakilisha Kristo mbele ya makanisa yao. Kwa mara nyingine tena, Immanuel aliindesha baiskeli yake kurudi nyumbani, akiwa mwenye mawazo na tafakari

nyingi. Kuna wazo jipya liliibuka mawazoni mwake. Mjadala wa leo ulisababisha aanze kuwaza juu ya kuwa na mke na watoto, kitu ambacho alikiweka kando kwa muda hapo awali.

Immanuel aliendelea kujiuliza. Mwanamke mcha Mungu, atakayetembea nami kwenye kazi hii takatifu—ambaye atanishauri na kushirikiana nami—atakuwa baraka, alijiwazia.

Immanuel alipokuwa akirudi nyumbani aliona familia kila eneo. Kwa mara ya kwanza aliwaona wake za watu wakifanya kazi kwa bidii na watoto wakicheza kwa furaha, ni kama vile macho yake yamefunguliwa. Aliendelea kuwaza juu ya familia. Nyumba inaweza ikawa ni sehemu nzuri kutekeleza ukarimu. Inaweza kuwa ni sehemu pia nzuri kwaajili ya kutembelea na kujenga urafiki na wale ambao wako kwenye hali ya uhitaji.

Immanuel alifika mwisho wa safari yake na kuiegesha baiskeli yake kwenye ukuta. Alifanya maamuzi ndani ya moyo wake, nitaanza kuomba kwaajili ya kupata mke, kisha akaingia kwenye nyumba ya wazazi wake.

# Sura ya Sita: Maswali

1. Sura hii imejaa maelezo juu ya vigezo ambavyo kiongozi wa kanisa anapaswa kuwa navyo. Andika maelezo kiasi mbele ya kila kigezo, kuelezea vile ulivyoelewa. Kama kuna viongozi wa kanisa jirani nawe mnaweza kujadiliana kwa pamoja.

    a. Kiongozi wa kanisa anapaswa kuwa na shauku takatifu kumtumikia Mungu kama mchungaji wa kanisa la Mungu:

b. Kiongozi wa kanisa ni mwamini mwenye ukomavu na muda wa kutosha kwenye wokovu:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c. Kiongozi wa kanisa aonyeshe uwezo wa kufundisha:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

d. Kiongozi wa kanisa huiongoza nyumba yake katika utaraibu mzuri:

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

e. Kiongozi wa kanisa anaonyesha mfano mwema wa ndoa ya kiungu kwa wale wanaomzunguka kwa matendo kama vile kumpenda mke wake:

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

f. Kiongozi wa kanisa huishi maisha ya uchaji kwenye jamii yake:

________________________________________________

________________________________________________

g. Kiongozi wa kanisa hujenga mahusiano na huenenda katika upole kwa wale wanaomzunguka:

h. Kiongozi wa kanisa hukua na kuendelea katika ukomavu kwenye maisha yake yote:

i. Kiongozi wa kanisa hulinda Uhuru wake kwa kujiepusha na kileo na fedha:

j. Kiongozi wa kanisa hatafuti kuwa tajiri kutokana na huduma yake:

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

2. Mwanafunzi mmoja aliuliza iwapo kiongozi wa kanisa anapaswa kuishi maisha makamilifu. Mwalimu alijibuje swali hilo?

# Sura ya Saba:

## Mfano wa Mchungaji

Immanuel hakukwea baiskeli yake Jumatatu iliyofuatia kuelekea darasani kwake. Badala yake alifanya kazi ya mchungaji. Mama mmoja, mzee kwa umri, wa pale kijijini kwake alifariki. Immanuel aliwahi kumtembea mara kadhaa wakati akiwa kwenye hali ya ugonjwa, akisoma na neno na kuomba pamoja naye. Bibi huyu aliyaishi maisha yake kwa kumpendeza na kumtumaini Kristo.

Immanuel hakuweza kufika darasani, lakini alitambua jukumu lililokuwa mbele yake ndiyo sababu hasa iliyompeleka hata kwenye hilo darasa. Anapaswa kuwachunga kondoo hata kwenye nyakati ngumu, kama hivi sasa.

Immanuel alipanda baiskeli yake na akaendesha kuelekea nyumbani kwa yule mama. Alisoma neno la Mungu na kuwashirikisha juu ya ahadi za Mungu kuhusu mbingu. Aliwasaidia kujiandaa kwaajili ya msiba na ibada ya maziko. Aliongea na kikundi cha wanawake waliokuwepo kanisani kuandaa chakula kwaajili ya wafiwa. Alimwelekeza mhazini wa kanisa lao dogo

afanye manunuzi ya chakula na kubeba sadaka kidogo ya upendo.

Siku zilizofuatia kwenye wiki, Immanuel alichukua nafasi yake ya kuongoza ibada ya msiba. Kwa kutumia kile alichojifunza darasani, alijisomea neno na kuona ahadi sita nzuri kabisa kuhusiana na mbingu, ambazo aliwashirikisha waombolezaji waliohudhuria.

Watu wa kijijini waligundua ya kwamba aliongea kwa huruma na mguso. Sauti yake ilipanda, na imani iliangaza kama nuru kwenye giza pale alipoanza kuzungumza juu ya mbingu na kurudi kwa mara ya pili kwa Bwana Yesu.

Baada ya kutembea pamoja na familia hii, kuhubiri kwenye msiba, na kuwafariji waombolezaji waliofika msibani, alijisikia hali ya kuchoka. Immanuel alijisikia hali ya kuchoka sana kuliko ile ambayo huipata atokapo kuchunga mifugo ya baba yake kwa kutwa nzima! Aligundua ya kwamba kila mara ambapo mchungaji huwahudumia watu kiroho hujimimina kwao.

Jumatatu iliyofuatia Immanuel alirudi darasani. Alichomoa Biblia yake, daftari na penseli, kama kawaida, wakati akiwasubiria wanafunzi wenzake wawasili.

Mwalimu alianza kufundisha kwa namna ya tofauti ambayo haikutarajiwa na wengi. "Leo,

darasa, hatutaenda kusoma Biblia kwa kina kama tulivyozoea kwenye wiki zilizotangulia. Leo nitawasimulia ushuhuda wa mchungaji mmoja maarufu katika historia. Ushuhuda huo uliyagusa maisha yangu."

Immanuel alipenda sana shuhuda, hakunyanyua penseli yake bali alikaa kwa umakini kwenye kiti chake, tayari kujifunza kutoka kwenye maisha ya huyu mchungaji mwingine.

Mwalimu alivuta dawati na kulisogeza mbele kidogo kisha akakaa. "Ninataka niwasimulie habari ya mchungaji mmoja aitwaye George Muller. Huyu aliishi miaka ya 1800 hivi. Vitabu vingi vimeandikwa kumuhusu japokuwa yeye aliandika kidogo sana kuhusiana na maisha yake. Watu wanapomuwaza George Muller humuwaza mtu wa mombi. Zaidi ya hapo, aliishi maisha ya kawaida, mchungaji aliyejitoa na kulijali kundi lake na kumtumikia Bwana.[2]"

"George alikulia Ujerumani, aliishi maisha ya uovu, kila mara aliitia aibu familia yake," mwalimu alieleza. "Alikiri ya kuwa amewahi kuiba, kusema uongo, na hata kucheza kamali. Hakuwahi kujifunza kuhusu Biblia nyumbani kwao kabisa na alihudhuria ibada za kanisa kwenye sikukuu kadhaa. Alipofikisha umri wa

miaka ishirini, rafiki yake mmoja alimwalika kwenye kipindi cha kujifunza Biblia. Kwa sababu fulani, japokuwa hakuwa ni mtu anayevutiwa na mambo ya namna hiyo, aliamua kwenda tu."

"George aliona ni ajabu kuona watu ambao hajawahi kukutana nao kwenye maisha walimsalimia kwa bashasha. Kipindi kilifuata mtiririko maalum. Waliokusanyika waliimba wimbo wa kitabuni, mtu mmoja miongoni mwao alipiga magoti na kuongoza maombi, na hatimaye, kifungu cha maandiko kikasomwa na kujadiliwa."

"George alijisikia kuchomwa moyo wake na yale maombi. Hajawahi kusikia maombi ya namna ile. Hayakuwa yamekaririwa kutoka kwenye kitabu cha maombi, bali yalitoka kwenye kilindi cha moyo wa mwombaji anayezungumza na mtu wanayefahamiana vyema. Mungu aliuhudumia moyo wa George kwa namna ya ajabu kupitia tukio hilo. Muda si mrefu, alianza kuhudhuria vipindi vya kujifunza Biblia mara kwa mara. Punde, alifanya uamuzi wa kumwamini Yesu na akaanza kukua kama mkristo."

Kama mimi vile, Immanuel alijiwazia mwenyewe. Sikuishi maisha ya utoto nikiwa mtukutu, lakini nilimwamini Yesu nikiwa kijana, kama huyu mchungaji, George Muller.

Alisogea mbele kwenye dawati lake, na kutaka kusikia zaidi.

“George alisoma sana habari za wamishionari, watu waliomwamini Yesu ambao husambaza habari njema kwenye maeneo mapya,” mwalimu aliendelea. “Alipata msukumo wa kuwa mmishionari na kusoma chuo cha Biblia nchini Ujerumani. Alianza kuhubiri nchini Uingereza akiwa kijana kwenye miaka ishirini na tano na alipofikisha miaka ishirini na saba alienda Bristol, Uingereza kutumika kama muhubiri kwenye kanisa. Hakuwa mmishionari lakini alitumika kama mchungaji mpaka alipofariki dunia akiwa na umri wa miaka tisini na mbili.”

Immanuel alisikia minong’ono kutoka kwa wanafunzi wenzake. Akajiunga nao, kushangaa namna ambavyo mchungaji anaweza kujimimina kiasi kile kwa zaidi ya miongo sita.

“Hiyo habari walau inatoa mwanga kuhusiana na maisha na kifo chake,” mwalimu alisema. “Lakini Geroge Muller alifahamika zaidi kwa kazi aliyoifanya na watoto yatima na shule za kikristo. Alianzisha shule 117, na kutoa elimu ya kikristo kwa zaidi ya watoto 120,000. Vituo vyake vililea zaidi ya watoto 10,000 muda wote wa uhai wa George.”

"Mnakumbuka tulipozungumza kuhusu kuepuka mtego wa kupenda fedha? Sikilizeni kwa umakini. Geroge alikuwa na sheria kali sana kuhusu uchangishaji fedha kwenye huduma yake. Alikusudia moyoni mwake tangu mwanzo ya kwamba kanisa, shule na vituo vyake havitachangisha fedha wala zawadi au msaada. Nini aliona kinatokea? Mungu kwa namna ya kimiujiza alikutana na mahitaji yao pasipo George kuwa na deni! Lakini pia alipokea fedha ambazo naye alizitoa kwa wamishionari. Geroge aliyaombea mahitaji yake, na Mungu alimpatia. Geroge kwa sasa anatambulika kama mtu wa maombi kwenye historia ya ukristo."

"Alipotimiza umri wa miaka sabini alianza kusafiri kwenye mataifa mengine uliwemnguni—nchi zaidi ya thelathini." Mwalimu alitulia. "Kitu gani kinachonivutia sana? Alitumia muda mwingi kuzungumza na wachungaji kwenye safari zake. Aliwapatia ujumbe uleule popote alipokwenda kwasababu aliwiwa kuhusu nafasi ya mchungaji wa kanisa la Mungu. Alifundisha maneno kumi yenye uzito kuhusiana na uchungaji."

Mwalimu alisimama na kuchukua kipande cha chaki. "Ninadhani mnapaswa kuyaandika haya," alisema. "Yanapaswa kufanana nanyi

kwa kiasi fulani kwa sasa. Nitaorodhesha ubaoni na tutajadiliana kidogo juu ya kila kipengele."

1) **Mchungaji ni lazima awe ni mtu aliyemwamini Yesu.**

"Biblia inatuelekeza kuhakikisha ya kwamba imani yetu iko sawa kabla hatujakubali nira ya uongozi wa kiroho," mwalimu alielezea. "Tunapaswa kuwa kweli tumezaliwa mara ya pili kwa Roho na kuwa na imani ya kweli na thabiti ndani ya Yesu Kristo. Hatuwezi kumpatia mtu mwingine kile tusichokuwa nacho, kwani tunaweza?" Mwalimu aliligeukia darasa na kuliuliza. "Tunaelewana mpaka hapo:

- Tunapokea wokovu kwa njia ya imani pekee, kwa neema ya Mungu?
- Yesu alikufa na kufufuka ili kulipa deni yetu ya dhambi?
- Ni njia pekee ya kwenda mbinguni?

2) **Mchungaji anapaswa kuwa na kina cha maarifa juu ya Yesu Kristo Bwana.**

"Yesu ndiye tunayemtumikia; kanisa haliwezi kuwepo bila Yeye. Tunahitaji Kumjua Yeye, kumwabudu Yeye, na

kumtumikia kwa mioyo yetu yote. Haya hayatokei kwa kufuata taratibu fulani za dini au kuwa sehemu ya kanisa fulani. Hii hutokea kwasababu tunamilikiwa na tunamjua Bwana Yesu mwenyewe."

3) **Mchungaji lazima adhihirishe ukuaji katika furaha na upendo.**

"Mnakumbuka tulizungumza vigezo vya mchungaji? Mchungaji hawezi kufanikiwa isipokuwa maisha yake yanadhihirisha tunda la maisha ya ukristo. Hili hudhihirika kwa njia ya furaha kutoka kwa Bwana, upendo kwa Mungu na watu wake, na ukuaji kama mkristo upendo na furaha ya Mungu lazima vitiririke bila unafiki kutokea kwenye maisha ya mchungaji."

4) **Mchungaji lazima alishe roho yake yeye mwenyewe.**

"Huduma ya kichungaji huwa ya manufaa kwa kanisa na washirika wake iwapo mchungaji huilisha roho yake mwenyewe kabla hajaanza kujaribu kulisha kanisa. Ni kwa namna gani anaweza kuambukiza imani na upendo kwa wengine isipokuwa vinatokea ndani ya moyo wake yeye

mwenyewe? Mnakumbuka mjadala wetu kuhusiana na hitaji la kuwa na muda wa kuomba na kusoma neno la Mungu? Hii huturuhusu tulishe roho zetu wenyewe, ili tuweze kuwalisha wengine."

5) **Lengo kubwa la mchungaji linapaswa kuwa maisha ya utakatifu.**

"Maisha binafsi ya mchungaji yanapaswa kuakisi maisha anayoyaonyesha kwenye hadhara," mwalimu alisema. "Mchungaji hapaswi kuigiza lolote. Anapaswa kuyaishi maisha yake kwa ukweli na uaminifu, akijilekeza katika kumpendeza Mungu kwa maisha yenye utiifu na utakatifu, badala ya fedha, cheo, hadhi, na faida binafsi na mambo yanayofanana na hayo."

6) **Taji inayomfunika mchungaji inapaswa kuwa ni unyenyekevu.**

"Hesabu 12:3, Kwenye Agano la Kale, inatuambia ya kwamba Musa aliishi maisha ya unyenyekevu kuliko mwanadamu yeyote kuwahi kutokea kwenye uso wa nchi. Hii inamaanisha Musa alitafuta kuyatenda mapenzi ya Mungu na kuwatumikia wengine

badala ya kujiwazia yeye mwenyewe. Je nasi tutaishi hivyo?"

7) **Ujumbe wa mchungaji unapaswa kupokelewa kutoka kwa Mungu.**

"Leo tunaweza kusikia jumbe kutoka kila mahala—kutoka kwa watu wengine, kutoka kwenye utamaduni wa dunia, na baadhi ya jumbe kutoka kwa shetani. Kila ujumbe ambao mchungaji anautoa unapaswa kutoka kwa Mungu na Neno lake pekee. Tunapokea ujumbe wa Mungu kwenye mioyo yetu wenyewe, tunatendea kazi kwenye maisha yetu wenyewe, na kisha tunawahubiria wengine."

8) **Ujumbe wa mchungaji lazima uyafafanushe maandiko.**

"Kuhubiri hakumaanishi kupiga moyowe, kufuata mtindo fulani maalum, kupiga makelele, au kujitengenezea jina sisi wenyewe. Kuhubiri ni kuelezea neno la Mungu kwa namna ambayo inawaruhusu watu kuyaelewa na kuyatenda mapenzi ya Mungu. Mahubiri yanaweza kutokea kwenye ngazi tofauti tofauti, njia rahisi

mpaka ya kina. Ukweli wa kawaida kutoka kwenye Biblia utalisha roho za watu."

9) **Mchungaji anapaswa kuwa na msukumo wa ndani wa neno la Mungu juu ya maisha ndani ya kanisa na kuondoa namna zozote zinazofuatisha mambo ya dunia.**

"Kwa urahisi kabisa, wachungaji wanapaswa kuchukua maelekezo na amri zao kutokea kwenye neno la Mungu badala ya kufuatisha dunia inayotuzunguka."

10) **Mchungaji anapaswa kuwa mwenye juhudi katika maombi.**

"George Muller aliishi huduma yake kwa mwendo huu. Kumbuka, maombi yako kama njia ambayo Mungu ameiweka ili kwayo watu wajipatie mambo wanayoyahitaji kwaajili ya maisha na huduma kutoka kwenye mkono wa Mungu."

Mwalimu aliweka chaki chini kisha akarejea kwenye kiti chake. "Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuwa – au anahitaji kuwa – George Muller. Tunayatazama maisha yake kama kielelezo cha mtumishi wa Mungu. Wachungaji

wengi wanaweza kutuonyesha namna ya kumtumikia Mungu kama wachungaji wacha Mungu. Nimewasimulia huu ushuhuda ili kuwapa hamasa kuiga mfano wa George Muller na kutafakari kwa kina kile unachokiona kwenye maisha ya wachungaji wa namna hii. Ndivyo nawe utakavyokuwa kielelezo cha kiungu kwa wengine kufuata!"

Kwenye mapumziko mafupi ya chai, Immanuel alitembea kueleka upande mwingine wa shule na kuegamia ukuta chini ya kivuli. Kulikuwa na jua kali na joto. Alipokuwa akipumzika, aliyanyanyua macho yake juu na kuomba.

"Bwana," alianza, moyo wake ukiwa katika unyenyekevu. "Sijui ni kwanini uliniita kuifanya kazi hii. Ninaona ni kazi kuu na takatifu sana. Unajua ya kwamba mimi ni kijana mdogo, lakini ninachojua ni kwamba ninakupenda na ninalipenda neno lako. Kanisa lako ni kila kitu kwangu. Unisaidie nilijenge na nikuletee utukufu. Unisaidie niipe kazi yako kipaumbele. Ninaomba unitunze na unipatie mahitaji yangu. Asante kwa kuniokoa. Unisaidie nilete wokovu kwa watu wengi zaidi kijijini kwetu. Ilinde kazi yako, Bwana. Yesu ung'are kwa watu wako wote."

Immanuel alikunywa chai kiasi, kwa moyo uliojaa shukurani na hali ya matarajio makubwa.

# Sura ya Saba: Maswali

1. Immanuel alikosa darasa moja ili aihudumie familia moja ya kanisani kwake iliyokuwa kwenye hali ya majonzi. Ni kwa namna gani alitendea kazi mambo aliyojifunza darasani ili kumsadia kutoa faraja kwa familia yenye huzuni?

2. Immanuel aligundua nini kuhusiana na kuwachunga watu wa Mungu baada ya kumaliza msiba? Je, nawe huwa unajisikia hivyo?

3. Mwalimu alihitimisha darasa lake kwa kuwasimulia wanafunzi wake ushuhuda wa George Muller na huduma yake. Mwalimu aliorodhesha mambo kumi ambayo George Muller aliwafundisha wachungaji. Ni mambo yapi kati ya hayo kumi ambayo unaguswa kujifunza zaidi?

4. Immanuel alisikia kuongozwa kuomba baada ya mafunzo ya darasani. Alijielekeza kwenye wito wa Mungu kwenye maisha yake na kiu yake ya kuendelea kuwa mnyenyekevu, kumruhusu Mungu atende kupitia yeye. Andika ombi lako fupi kama sehemu ya mwitikio wako baada ya kujifunza yote hayo kwenye kitabu hiki.

# Hitimisho

Kijana Immanuel aliianza safari yake kwa kumwamini Yesu Kristo kumuokoa kutoka kwenye hali yake ya dhambi. Kisha akaingia kwenye njia iliyompelekea kuwa mtu wa maombi na neno la Mungu. Alidumu katika kufundisha na kuongoza kanisa la Mungu—mchungaji wa kweli.

Immanuel alitambua wazi ya kwamba safari yake ilianza akiwa kijana na hivyo alaipaswa kujifunza mengi. Alitumia kila fursa ya ukuaji ambayo ilikuja mbele yake na alitendea kazi kila hatua ya mafundisho aliyoyapokea. Aliahidi kufanya kila liwezekanalo kuwa bora katika kumtumikia Mungu na watu wake. Mungu ainue wengi kama kijana huyu!

Je, uko tayari kuipokea changamoto ya uchaji na kutembea katika nyayo za miguu ya Immanuel? Je, utachagua njia ya wokovu na kumfuata Mungu, ili uwachunge wengine?

# Dondoo za Mwisho

1 https://www.jesusfilm.org.

2 Arthur T. Pierson, *George Muller of Bristol: His Life of Prayer and Faith* (Kregel Publications, 1999), tazama hususani kuanzia ukurasa 314 kuendelea.